# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

# HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

**MHESHIMIWA**
**RAHMA KASSIM ALI (MBM)**

## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**JUNI, 2026**

**UONGOZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI ZANZIBAR**




Mhe. Rahma Kassim Ali (MBM)
Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi



Mhe. Salha M. Mwinjuma
Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi



Ndg. Khadija Kh. Rajab
Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi



Ndg. Mhaza Gh. Juma
Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi



Ndg. Bakari A. Bakari
Afisa Mdhamini



Ndg. Noah S. Said
Mkurugenzi Uendeshaji na Utumishi



Ndg. Makame S. Ali
Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti



Ndg. Hannat B. Hamad
Mkurugenzi Maendeleo ya Makaazi



Ndg. Mussa K. Bakari
Katibu Mtendaji Kamisheni ya Ardhi



Ndg. Sultan S. Suleiman
Mkurugenzi Mkuu Shirika la Nyumba



Ndg. Fatma M. Omar
Mwenyekiti Mahkama ya Ardhi



FRV. Tahir M. Omar
Mthamini Mkuu wa Serikali

## YALIYOMO


UTANGULIZI ............................................................................................. 1
MUUNDO WA WIZARA.................................................................................. 3
MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI.................................................................................................. 3
MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026. .................................................. 4
MUHTASARI WA MAPATO ........................................................................ 4
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA MWELEKEO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027. ............................................................................................ 6
PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI ....................... 6
PROGRAMU NDOGO SN020101: URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI;......................................................................................... 7
PROGRAMU NDOGO SN020102: UTAWALA NA UENDESHAJI. ................................................................................................ 11
PROGRAMU NDOGO SN020103: URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA. ............................................................................. 14
PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI ........................ 17
PROGRAMU NDOGO SN020201: USIMAMIZI WA ARDHI .............. 18
HN02020108: UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI......................... 18
HN02020107: KUSIMAMIA NA KUIDHINISHA RIPOTI ZA UTHAMINI .................................................................................................. 20
HN02020101: UPANGAJI NA USIMAMIZI WA ARDHI ....................... 22
PROGRAMU KUU PN0203: MAENDELEO YA MAKAAZI ............... 28
PROGRAMU NDOGO SN020301: MAENDELEO YA MAKAAZI................................................................................................. 29
HUDUMA HN02030102: USAJILI WA MAJENGO NA JUMUIYA ZA KONDOMINIO. ........................................................................... 29
HN02030105 UTATUZI WA MIGOGORO KWA WAPANGAJI WA NYUMBA. ............................................................................................ 32
SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR.................................................... 33

VIPAUMBELE VYA BAJETI YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027. .... 38
MAOMBI YA IDHINI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027. .... 38
SHUKRANI .... 39
HITIMISHO .... 41
VIAMBATISHO .... 43

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI MHESHIMIWA RAHMA KASSIM ALI (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR.**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika;** kwa ruhusa yako, naomba kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika;** Naanza Hotuba yangu kwa kumshukuru Allah (S.W) kwa kuendelea kutupatia neema yake ya uhai na uzima tukaweza kuhudhuria katika kikao cha kujadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii.

3. **Mheshimiwa Spika;** Uongozi na Wafanyakazi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi unatoa Shukrani na pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa tena kuongoza taifa letu katika awamu nyengine, ushindi wake ni ishara ya imani kubwa waliyonayo Watanzania katika uongozi wake mahiri, wenye busara na unaolenga maendeleo endelevu ya nchi. Tunatambua mchango wake mkubwa katika kuhakikisha anaweletea maendeleo Wananchi wa Tanzania. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumlinda pamoja na kumsimamia katika kutekeleza majukumu yake na nawaomba Watanzania waendelee kumuamini katika kuingoza Nchi yetu ili aendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

4. **Mheshimiwa Spika;** Kipekee, nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa tena kuongoza Nchi yetu kwa kipindi cha pili cha awamu ya nane kwa ushindi wa kishindo kwa **asilimia 74.8.** Uongozi wake umeleta mchango mkubwa katika kuimarisha Sekta ya Ardhi na Makaazi, hususan katika kuhakikisha matumizi bora ya ardhi, upangaji wa Miji na Vijiji, pamoja na kuboresha Makaazi kwa kuwapatia Wananchi nyumba bora na za kisasa na kuhakikisha maendeleo endelevu ya Nchi kupitia Sekta hizi

yanapatikana. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu, afya, hekima, busara na ustahamilivu katika kuingoza Nchi yetu pamoja na kumuwezesha kufikia azma yake ya kuiletea Maendeleo kwa kasi zaidi.

5. **Mheshimiwa Spika;** Napenda kumpongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamo wa Pili wa Rais Zanzibar kwa kuendelea kuaminiwa kushika nafasi hiyo na kumsaidia Mheshimiwa Rais katika usimamizi wa utendaji wa Serikali. Uteuzi huo ni ishara ya imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais kwake, na ni uthibitisho wa namna anavyomsaidia katika kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar pamoja na kusimamia na kufuatilia kwa karibu shughuli na Miradi ya Serikali kwa ufanisi na weledi. Ni matumaini yetu kua ataendelea kutekeleza majukumu yake kwa bidii, uadilifu na uzalendo mkubwa kwa manufaa ya maendeleo ya Zanzibar na Ustawi wa Wananchi wake. Tunamuomba Allah (S.W) azidi kumpa nguvu, busara na hekima katika kutekeleza majukumu yake makubwa ya uongozi.

6. **Mheshimiwa Spika;** Kwa namna ya pekee, napenda kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wasaidizi wako kwa busara na Hekima mnazozitumia katika kuliongoza Baraza hili. Vilevile, naomba kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Pia napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA ya Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Mihayo Juma N'unga; Makamo Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanaidi Kassim Mussa pamoja na Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA kwa mashirikiano makubwa wanayoendelea kutupatia tangu walipoanza kufanya kazi na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi. Ni dhahiri kua ushirikiano wao umekuwa ni chachu muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara, hususan katika kusimamia na kuendeleza Sekta ya Ardhi na Makaazi. Wizara inaahidi kua ushauri na maelekezo tunayopatiwa tutaendelea kuyafanyia kazi kwa umakini, umahiri na ufanisi, ili kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa manufaa ya Wananchi na Nchi kwa ujumla.

## MUUNDO WA WIZARA

7. **Mheshimiwa Spika;** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imeundwa na Sekta ya Ardhi na Sekta ya Makaazi inayojumuisha Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango Sera na Utafiti, Idara ya Maendeleo ya Makaazi pamoja na Ofisi Kuu Pemba. Aidha, Wizara ina Taasisi tatu (03) na Shirika moja ambazo ni Kamisheni ya Ardhi (COLA), Mahakama ya Ardhi, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali pamoja na Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC). Vilevile, Wizara ina Bodi Tendaji moja ambayo ni Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba.

## MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

8. **Mheshimiwa Spika;** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imepangiwa na inatekeleza majukumu makuu yafuatayo:-

   1. Kutunga na kusimamia utekelezaji wa Sera za Kisekta na Sheria Zinazohusiana na Ardhi, Nyumba na Makaazi;

   2. Kushajihisha na Kutekeleza Upatikanaji wa Makaazi Bora na Nafuu kwa Wananchi;

   3. Kusimamia Utambuzi, Usajili na Umiliki wa Ardhi Nchini;

   4. Kufanya Tafiti Zinazohusiana na Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makaazi;

   5. Kutayarisha na Kusimamia Utekelezaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Nchini Mijini na Vijijini;

   6. Kusimamia Rasilimali Watu, fedha na Rasilimali Nyenginezo za Wizara.

9. **Mheshimiwa Spika;** baada ya utangulizi huo, naomba sasa uniruhusu kuelezea utekelezaji wa Kazi za Kawaida na Maendeleo za Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Muelekeo wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.**

**MUHTASARI WA MAPATO**

10. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 17,778,918,136** ambapo **TZS Bilioni 7,614,810,000** kutoka vyanzo vilivyomo ndani ya Wizara {Ada ya Mahakama, Usajili wa Kondominio, Vibali vya Ujenzi na Ada ya Uthamini} na **TZS Bilioni 10,164,108,136** kutoka vyanzo vya Kamisheni ya Ardhi {Uhaulishaji wa Ardhi, Ada ya Upimaji na ramani, Ada ya Usajili wa Ardhi, Ada ya Uthamini na Miongozo ya Matumizi ya Ardhi}.

11. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Miezi Tisa (Julai-Machi 2025/2026) Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 13,299,916,115** ambapo **TZS Bilioni 5,725,107,500** kutoka katika vyanzo vya mapato vya Wizara na **TZS Bilioni 7,574,808,615** kutoka vyanzo vya mapato vya Kamisheni ya Ardhi.

12. **Mheshimiwa Spika;** Wizara hadi kufikia Machi, 2026, imekusanya jumla ya **TZS Bilioni 7,238,720,358** sawa na **asilimia 54.4** kwa kipindi cha Miezi Tisa na **asilimia 40.7** kwa mwaka. {**TZS Bilioni 1,152,887,436** kutoka vyanzo vya mapato vya Wizara sawa na **asilimia 20.1** ya makadirio ya makusanyo ya Miezi Tisa na **asilimia 15.1** ya makadirio ya Mwaka na **TZS Bilioni 6,085,832,922** kutoka vyanzo vya Kamisheni ya Ardhi sawa na **asilimia 80.0** ya makadirio ya makusanyo ya Miezi Tisa na **asilimia 60** ya makadirio ya Mwaka}. **Kiambatanisho nambari 1 (a) kinafafanua.**

13. **Mheshimiwa Spika;** Sababu kuu zilizopelekea kushuka kwa makusanyo yatokanayo na vyanzo vya Wizara ni pamoja na muingiliano wa majukumu ya utoaji wa vibali vya ujenzi ambavyo pia vinatolewa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, udogo wa thamani ya Miradi ya Kondominio iliyosajiliwa pamoja na kusita kuyapima na kutoa Mikataba ya Ukodishwaji wa Ardhi katika maeneo ya ukanda wa Bahari kwa upande wa Pemba kutokana na zoezi la kuyapanga vizuri maeneo hayo.

**MUHTASARI WA MATUMIZI**

14. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ilipangiwa kutumia Jumla ya **TZS Bilioni 345,485,900,000** kati ya fedha hizo **TZS Bilioni 5,799,600,000** Mishahara **{TZS Bilioni 2,734,600,000** Mishahara kwa Idara zilizo chini ya Wizara na **TZS Bilioni 3,065,000,000** zilitengwa kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara ya Kamisheni ya Ardhi}. **TZS Bilioni 3,493,600,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya uendeshaji wa Ofisi kwa Idara zilizo chini ya Wizara na **TZS Milioni 507,700,000** ni Ruzuku kwa ajili ya Taasisi za Wizara, **TZS Billioni 335,685,000,000** kwa ajili ya kazi za Maendeleo na **asilimia 50** ni matumizi yanayotokana na zuio (Retention) ya makusanyo yanayotokana na vyanzo vya Kamisheni ya Ardhi.

15. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Miezi Tisa, Wizara ilikadiriwa kutumia **TZS Bilioni 296,556,021,430** kati ya fedha hizo **TZS Bilioni 7,689,871,430** kwa utekelezaji wa Kazi za Kawaida {**TZS Bilioni 2,050,949,750** Mishahara kwa Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Bilioni 2,956,171,680** Matumizi ya Kawaida ya uendeshaji wa Ofisi kwa Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Milioni 384,000,000** Ruzuku kwa ajili ya Taasisi za Wizara na **TZS Bilioni 2,298,750,000** Ruzuku ya Mishahara ya Kamisheni ya Ardhi} na **TZS Billioni 288,866,150,000** kwa Kazi za Maendeleo.

16. **Mheshimiwa Spika; pia,** Wizara kupitia Kamisheni ya Ardhi ilikadiriwa kutumia **asilimia 50** ya makusanyo kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Kamisheni ya Ardhi.

17. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya **TZS Bilioni 5,595,947,568** zimepatikana **{TZS Bilioni 1,100,229,308** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Bilioni 4,343,883,260** kwa ajili ya Mishahara **{TZS Bilioni 2,065,772,748** ni Mishahara ya Idara za Wizara na **TZS Bilioni 2,278,110,512** kwa ajili ya Ruzuku ya Mishahara ya Kamisheni ya Ardhi}, **TZS Milioni 151,835,000** kwa ajili ya Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida kwa Taasisi za Wizara, na hakuna fedha zilizopatikana kwa ajili ya Kazi za Maendeleo sawa na

**asilimia 1.9** kwa makadirio ya Miezi Tisa na **asilimia 1.6** kwa makadirio ya mwaka. **Kiambatanisho nambari 1 (b) kinafafanua.**

## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA MWELEKEO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.

18. **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara imetekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu tatu ambazo ni Programu PN0201: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Programu PN0202: Usimamizi wa Ardhi na Programu PN0203: Maendeleo ya Makaazi.

## PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

19. **Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu PN0201 ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ina jukumu la kuimarisha uratibu katika utekelezaji wa kazi za Wizara. Programu hii inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo ni Programu ndogo SN020101 ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti; Programu Ndogo SN020102 ya Uendeshaji na Utumishi na Programu Ndogo ya SN020103 ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

20. **Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Kuu PN0201 ilikadiriwa kukusanya **TZS Bilioni 2,725,810,000** kutokana na vyanzo vyake vya Mapato {Ada ya Mahakama, Usajili wa Miradi ya Kondominio na Vibali vya Ujenzi} na **TZS Bilioni 2,044,357,500** zilikadiria kukusanywa kwa Miezi Tisa.

21. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, fedha zilizokusanywa ni **TZS Milioni 279,929,100** sawa na **asilimia 13.7** kwa Kipindi cha Miezi Tisa na **asilimia 10.3** kwa Mwaka.

22. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Kuu PN0201 ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 39,965,904,600 {TZS Bilioni 2,145,768,600** Mishahara ya Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Bilioni 2,255,136,000** Matumizi ya Kawaida ya Idara zilizo chini ya Wizara na **TZS Bilioni 35,565,000,000** kazi za Maendeleo}.

23. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Miezi Tisa Programu ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 35,378,306,185 {TZS Bilioni 1,596,918,283** Mishahara kwa Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Bilioni 1,917,215,997** Matumizi ya Kawaida kwa Idara zilizo chini ya Wizara na **TZS Bilioni 31,864,171,905** kwa Kazi za Maendeleo}.

24. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya **TZS Bilioni 2,435,884,399.1** zimepatikana **{TZS Bilioni 1,640,019,233** Mishahara kwa Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Milioni 795,865,166.1** Matumizi ya Kawaida kwa Idara zilizo chini ya Wizara na hakuna fedha iliyoingia kwa Kazi za Maendeleo}. sawa na **asilimia 6.9** kwa Miezi Tisa na **asilimia 6.1** kwa Mwaka.

25. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Kuu PN0201 kupitia Programu zake ndogo tatu zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

**PROGRAMU NDOGO SN020101: URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI;**

26. **Mheshimiwa Spika;** Progamu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na ina jukumu la kuratibu na kusimamia utayarishaji na utekelezaji wa Sera, Sheria, Bajeti, Miradi na Mipango ya Taasisi zote zilizomo ndani ya Wizara. Pia, Programu hii inaratibu ufanyaji wa tafiti, ufuatiliaji na Tathmini na kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Vile vile, Programu hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilipewa jukumu la kuratibu shughuli za Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Ujenzi (DCU).

27. **Mheshimiwa Spika;** hadi kufikia Machi, 2026, Programu ndogo imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imeratibu utekelezaji wa Miradi inayotekelezwa na Wizara kama ifuatavyo:-

   a. **Programu ya Kuendeleza Makaazi.** Programu hii inahusisha Ujenzi wa Nyumba za Makaazi katika Maeneo mbalimbali Unguja na Pemba na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeweza kufanya uratibu wa utekelezaji wa Miradi ya Chumbuni, Kisakasaka,

Nyamanzi, Mombasa kwa Mchina, Mabaoni, Mkungu Malofa sambamba na Ujenzi wa Hotel na Maeneo ya Biashara katika eneo la Gofu.

b. **Mradi wa Kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi Kisiwani Pemba kupitia Programu ya BIG -Z.** Mradi unahusisha uandaaji wa Master Plan ya Kisiwa cha Pemba pamoja na kuandaa Mipango Kina kwa Miji Minne ikiwemo Chake Chake, Mkoani, Wete na Micheweni. Kwa sasa Mshauri elekezi wa kazi hiyo anaendelea na hatua ya kuandaa rasimu ya awali (First Draft) ya Mpango huo na inatarajiwa kuwasilishwa mwezi wa Juni, 2026 Wizarani. Aidha, Mpango unatarajiwa kukamilika mnamo mwezi Disemba, 2026.

Vilevile, kupitia Programu ya BIG -Z, Wizara inaendelea na shughuli za uandaaji wa Kanuni za Ujenzi (Building Code) zitakazotumika katika uendelezaji wa Sekta ya Ujenzi nchini. Hivi sasa, Mshauri elekezi anaendelea na kuandaaa taarifa ya hali halisi ya Zanzibar katika masuala ya ujenzi ambapo taarifa hiyo imeshawasilishwa Wizarani.

Aidha, kupitia Programu ya BIG-Z, Wizara inaendelea na uratibu wa Mradi wa Mfumo wa kuhifadhi Taarifa za Taifa za Kijografia ZanSDI, kwa sasa Mfumo huo upo katika hatua za majaribio.

c. **Mradi wa Mfumo wa Usajili wa Taarifa za Ardhi (LARIS)** .Mradi una lengo la kuanzisha Mfumo utakaounganisha kidijitali taarifa za ardhi katika umiliki, Upimaji, Ramani, Mipango Miji, Uthamini, Usajili na matumizi mengine ya Ardhi na bahari ndani ya mipaka ya Zanzibar sambamba na kufanya utambuzi kwa maeneo 25,000. Kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeratibu maombi ya kibali cha upigaji wa Picha za Anga, ushiriki wa utiaji saini Mkataba wa kifedha pamoja na kumtafuta Mshauri elekezi wa kusimamia utekelezaji wa Mradi huo. Hatua inayoendelea kwa sasa ni kukamilisha taratibu za dhamana za kibenki (Bank Guarantee) ili utekelezaji uweze kuendelea.

ii. Imeendelea na ukamilishaji wa utayarishaji wa Sera ya Miji na Maendeleo ya Makaazi ambapo rasimu ya Sera hiyo imeshawasilishwa katika Kikao cha Baraza la Mapinduzi na kwa sasa inaendelea na hatua nyengine ili iweze kuchapishwa na kusambazwa kwa wadau kwa ajili ya matumizi.

iii. Imeratibu matayarisho ya mapitio ya Sera ya Ardhi ya mwaka 2018 kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka Chuo cha Ardhi Dar es Salaam kwa ajili ya uandaaji wa Sera ya Ardhi ya mwaka 2026. Taarifa ya awali ya uandaaji wa kazi hiyo (Inception Report) imeshawasilishwa Wizarani.

iv. Imeratibu uandaaji wa Rasimu ya Hati ya Makubaliano baina ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar na Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es Salaam ili kuimarisha utendaji katika masuala ya Ardhi na Makaazi.

v. Imeendelea kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2027 hadi 2029 ambapo hatua za awali za mapitio hayo zimeshakamilika na hatua inayofuata ni kuwasilishwa katika Kamati Tendaji ya Wizara kwa kupatiwa maoni na hatimae kuwasilishwa katika Kamati ya Uongozi ya Wizara ili uweze kutumika.

28 **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Idara ya Mipango pia .ilipewa jukumu la kuratibu shughuli za Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Ujenzi (DCU) ambapo kwa kipindi cha Julai – Machi 2026, Kamati imefanikiwa kufanya shughuli zifuatazo: -

1. Imefanya vikao vya Wataalamu vya kuchambua na kupitisha maombi ya vibali vya ujenzi na kufanikiwa kupitisha na kutoa vibali 38 vya ujenzi wa majengo mapya, ujenzi wa Majengo yanayoendelea pamoja na Miradi ya Maendeleo kupitia ZIPA. Kati ya hivyo, Unguja Vibali 09, Pemba vibali 2 na kupitia ZIPA vibali 27 vimetolewa. Vilevile, DCU kwa upande wa Pemba imeratibu utaoji wa vibali vya ujenzi wa Minara ya mawasiliano 17 ambavyo vimetolewa kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

2. Kamati ya DCU imefanya ukaguzi wa kawaida wa kufuatilia vibali vya ujenzi vinavyotolewa pamoja na kuangalia Wananchi kama wanajenga kulingana na vibali walivyoombea pamoja na kutoa indhari na kuwachukulia hatua wale wote wanaojenga bila ya kukata vibali au

kwenda kinyume na vibali walivyopewa wakati wa ujenzi wao. Ukaguzi huo umefanyika kwa Wilaya ya Mjini kwa maeneo ya (Mlandege, Kisiwandui, Kikwajuni, Mikunguni, Mpendae na Kilimahewa);Wilaya ya Kati (Uroa, Pongwe, Jumbi, Chwaka, Kikungwi, Tunguu na Ubago); Wilaya ya Kusini (Michamvi, Bwejuu, Paje Makunduchi na Jambiani); Wilaya ya Magharibi 'B' (Fuoni Uwandani, Fuoni Mambosasa, Taveta, Kijitoupele, Bweleo, Dimani, Tomondo na Kombeni) na Wilaya ya Kaskazini 'A' (Nungwi, Matemwe na Pwani Mchangani). Aidha, kupitia ukaguzi huo, Kamati imefanikiwa kuvunja baadhi ya maeneo ikiwemo Mabanda, Pongwe katika Wilaya ya Kati na Shakani Wilaya ya Magharibi B.

29. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/26, Programu hii ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 2,610,010,000** kutokana na Ada za Vibali vya Ujenzi. Kwa kipindi cha Miezi Tisa Programu ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 1,957,507,500** kwa Miezi Tisa.

30. **Mheshimiwa Spika;** hadi kufikia Machi 2026, fedha zilizokusanywa ni **TZS Milioni 276,580,700** sawa na **asilimia 14.1** ya makadirio ya makusanyo kwa Miezi Tisa na **asilimia 10.6** ya makadirio ya Mwaka.

31. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, jumla ya **TZS Bilioni 36,629,195,200** iliidhinishwa kutumika kwa utekelezaji wa Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti **{TZS Milioni 260,795,200** Mishahara, **TZS Milioni 803,400,000** Matumizi ya Kawaida na **TZS Bilioni 35,565,000,000** kazi za Maendeleo}.

32. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Miezi Tisa Programu kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 32,719,418,305 {TZS Milioni 195,596,400** Mishahara ya Idara, **TZS Milioni 659,650,000.00** Matumizi ya Kawaida **TZS Bilioni 31,864,171,905** kwa Kazi za Maendeleo}.

33. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya **TZS Milioni 289,034,656.1** zilipatikana **{TZS Milioni 143,290,500** Mishahara, **TZS Milioni 145,744,156.1** Matumizi ya Kawaida na hakuna fedha iliyoingia kwa ajili ya Kazi za Maendeleo} sawa na **asilimia 0.9** kwa Miezi Tisa na **asilimia 0.8** ya makadirio kwa mwaka.

**34. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti itaendelea kuandaa na kuzifanyia mapitio Sera na Sheria za Wizara. Sera moja itaendelea kufanyiwa mapitio (Sera ya Ardhi) na Sheria 3 (Sheria ya Sekta Milki, Sheria ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali na Sheria ya Mabaraza ya Ardhi);

Aidha, Program itaratibu mapitio na uandaaji wa Kanuni 5 za utekelezaji wa Sheria za Wizara (Kanuni ya Sheria ya Kamisheni ya Ardhi ya mwaka 2015, Kanuni ya Sheria ya Matumizi ya Ardhi namba 12 ya mwaka 1992, Kanuni ya Sheria ya Upimaji, Kanuni ya Sheria za Mipango Miji na Kanuni ya Sheria ya Usajili wa Ardhi namba 10 ya mwaka 1990). Vile vile, Proramu itafanya tafiti moja, itaendelea kukusanya takwimu za Sekta ya Ardhi, Makaazi na Nyumba; itafanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Miradi na Programu za Wizara na kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makaazi. Pia, Program itaratibu na kuandaa dhana za Miradi na kuwasilisha kwa Wasihirika wa Maendeleo kwa ajili ya kupata ufadhili wa kuendleza sekta ya Ardhi na Makaazi.

**35. Mheshimiwa Spika;** katika kujenga uwelewa kwa Wananchi juu ya mambo yanayohusu Sekta ya Ardhi pamoja na kupunguza migogoro ya sekta hiyo katika jamii. Programu kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi itaratibu na kusimamia Kliniki za Ardhi zinazoendelea kufanyika katika Wilaya zote Unguja na Pemba.

**36. Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Programu kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 922,402,000** ambapo **TZS Milioni 269,120,000** Mishahara ya Idara, **TZS Milioni 653,282,000** kwa Kazi za Matumizi ya Kawaida.

**PROGRAMU NDOGO SN020102: UTAWALA NA UENDESHAJI.**

**37. Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ina jukumu la kusimamia uendeshaji wa shughuli za Wizara, usimamizi wa rasilimali watu kwa kuandaa Mipango ya kuwajengea uwezo Watumishi, kuimarisha mazingira bora ya kazi, kushughulikia haki na stahiki za

Watumishi, kuhakikisha upatikanaji wa Watendaji wa kutosha na wenye sifa ndani ya Wizara na Taasisi pamoja na kusimamia nidhamu kwa Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Hadi kufikia Machi, 2026, imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imelipa stahiki za Wafanyakazi 30 (Wafanyakazi (20 )wamelipwa posho la likizo, Wafanyakazi (3) wamelipwa posho la ufiwa na Wafanyakazi (7) wamepatiwa posho la kufanya kazi baada ya saa za kazi (overtime).

ii. Imefanya upimaji wa Watumishi (30) ambapo wote walipatiwa nyongeza za Mshahara pamoja na Mtumishi mmoja kupandishwa Daraja baada ya kurudi masomoni. **Kiambatanisho nambari 2 kinafafanua.**

iii. Imegharamia mafunzo ya muda mrefu Mfanyakazi (1) na Wafanyakazi 21 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kiambatanisho nambari 3 (a) na 3 (b) kinafafanua.

iv. Imetengeneza Habari 27 na kuzirusha hewani kupitia vyombo vya habari na Mitandao ya kijamii. Aidha, Makala 2 zimeandaliwa kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya utekelezaji wa shughuli za Wizara.

v. Imesimamia upatikanaji wa huduma za kiofisi ikiwemo malipo ya umeme, vifaa vya kuandikia, ulinzi, usafi, huduma za posta na upatikanaji wa maji safi na salama, kwa lengo la kuhakikisha shughuli za Wizara zinatekelezwa kwa ufanisi.

vi. Imesimamia upatikanaji wa usafiri kwa kazi za Ofisi kwa ajili ya shughuli za Ofisi kwa kufanya matengenezo ya vyombo vya usafiri na ununuzi wa mafuta.

vii. Imesuluhisha na kuipatia ufumbuzi Migogoro ya Ardhi 18 kati ya Migogoro 35 iliyowasilishwa kwa Kamati ya Usuluhishi wa Migogoro ya Wizara na migogoro 17 inaendelea na hatua ya kufuatilia utatuzi wa Migogoro hiyo.

viii Jumla ya hoja na changamoto 56 zilizowasilishwa na Wananchi kupitia Mfumo wa Sema na Rais Mwinyi (SNR) kati ya hizo hoja 34 zimepatiwa ufumbuzi, hoja 8 zimeondolewa kutokana na kukosa vithibitisho kamili, hoja 10 zimehamishwa kutoka Wizara kwenda taasisi husika kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi na hoja 4 zinaendelea na hatua.

viii. Inaendelea kusimamia miundombinu ya TEHAMA ya Wizara pamoja na kuboresha Kitengo cha TEHAMA kwa kuandaa ripoti ya tathmini kuhusu uboreshaji wa miundombinu hiyo na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA. Aidha, kupitia Kitengo cha TEHAMA, Wizara imefanikiwa kuandaa dhana za awali kwa ajili ya uandaaji wa Mifumo, ikiwemo Mfumo wa Mthamini Mkuu wa Serikali, Mfumo wa Usajili wa Migogoro ya Ardhi, Mfumo wa Usajili na Ufuatiliaji wa Kesi za Ardhi kwa Mahakama ya Ardhi na Mfumo wa Sekta Milki.

**38.** **Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha 2025-2026, Programu ya Utawala na Uendeshaji iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 2,053,245,200 (TZS Bilioni 1,440,835,200** Mshahara ya Idara na **TZS Milioni 612,410,000** Matumizi ya Kawaida).

**39.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Miezi Tisa, Programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 1,588,122,150 (TZS Bilioni 1,068,214,233** Mishahara na **TZS Milioni 519,907,917** Matumizi ya Kawaida).

**40.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi 2026, fedha zilizopatikana ni **TZS Bilioni 1,455,480,782.5 (TZS Milioni 1,154,390,709.5** Mishahara na **TZS Milioni 301,090,073** Matumizi ya Kawaida) sawa na **asilimia 91.7** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 70.9** kwa mwaka.

**41.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu ndogo ya Uendeshaji na Utumishi itaratibu shughuli za uendeshaji na usimamizi wa rasilimali za Wizara; itasimamia uajiri Wafanyakazi 10 itafanya upimaji wa Watendaji kwa Wafanyakazi 85, itawajengea uwezo wafanyakazi (35) kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu (5) na muda mfupi (30) na kuwapatia stahiki zao kwa mujibu wa taratibu za Utumishi; itafanya mapitio ya Mkataba wa huduma kwa wateja na itaratibu mapitio ya miundo na majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ili kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa kazi na kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara.

**42.** **Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako kuidhinisha **TZS Bilioni 2,343,084,000** kati ya hizo **TZS Milioni 1,451,456,000** Mishahara na **TZS Milioni 891,628,000** Kazi za Kawaida.

**PROGRAMU NDOGO SN020103: URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA.**

**43.** **Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia Utawala na Mipango ya kazi zote za Wizara kwa upande wa Pemba ikiwemo Programu na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2026, Programu hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Programu kwa kushirikiana na Idara na Taasisi za Wizara imefanya ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo, Shughuli za Wizara pamoja na Miradi ya Kondominio kama ifuatavyo:-

a. Mradi wa Condo Hotel uliopo Wambaa Mkoani (Coco Lagon) kwa lengo la kuhakiki maombi ya kusajili ramani.

b. Mradi wa Jengo la Ofisi ya Shirika la nyumba pamoja na Makaazi lililopo Machomane kwa Kamanda ambalo limekamilika na kuzinduliwa katika Sherehe za kuadhimisha miaka 62 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

c. Mradi wa Jengo la Biashara na Makaazi liliopo Mkungumalofa Mabatini awamu ya pili.

d. Mradi wa ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Biashara uliopo Mfikiwa Mabaoni.

e. Eneo la Utambuzi wa Ardhi Mfikiwa ambapo zoezi hilo limekamilika.

f. Mradi wa ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Biashara uliopo Polisi line Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

ii. Imefanikiwa kutoa vibali viwili (2) vya ujenzi kupitia Kamati ya Usimamizi wa Vibali vya Ujenzi (DCU) pamoja na kuratibu zoezi la utaoji wa vibali vya ujenzi wa minara 17.

iii. Imefanikiwa kufanya ziara katika maeneo ya Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi Mvumoni, Micheweni na Wete yanayoendelezwa na Mradi wa International Consultants and Technology (ICT) wenye lengo la utayarishaji wa Mpango wa Ardhi Kisiwani Pemba (Pemba Master Plan) na kufanya ziara nyumba ya Maendeleo ya Mtemani ambayo ilipata ajali

ya moto pamoja na kumpatia fomu ya Kondominio kwa ajili ya kujisajili na kupata umiliki Kisheria.

iv. Imepokea Migogoro mipya ya Ardhi 12 kupitia Kamati ya Usuluhishi na Utatuzi wa migogoro, na kufanya kua na jumla ya migogoro 30 ukijumuisha na migogoro ya awali 18, ambapo imeweza kuitolea ushauri na suluhu migogoro 15 na kwa sasa Kamati inaendelea na ufuatiliaji wa migogoro 15.

v. Imewapatia Stahiki Wafanyakazi ikiwemo malipo ya safari, mafao ya ufiwa kwa Mfanyakazi mmoja (1), likizo kwa Wafanyakazi (9) na malipo ya posho la malipo baada ya saa za kazi kwa Wafanyakazi (16). Vilevile, imewapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi (5) na Wafanyakazi (3) wamepatiwa Mafunzo ya Muda Mrefu,

vi. Imefanya matengenezo ya Vyombo vya usafiri, kununua vifaa vya Ofisi na kulipa huduma za uendeshaji wa Ofisi zikiwemo umeme, mafuta pamoja na vifaa vya kuandikia.

44. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu ndogo ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 115,800,000** kwa mwaka na **TZS Milioni 86,850,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa kutokana na vyanzo vyake vya mapato ikiwemo Ada ya vibali vya ujenzi, Ada ya Mahakama na Ada ya usajili wa kondominio.

45. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **TZS Milioni 3,348,400** zimekusanywa sawa **asilimia 3.9** ya makadirio ya Miezi Tisa na **asilimia 2.9** ya mwaka. Asilimia hii imeshuka kutokana na muingiliano wa ukusanyaji wa mapato kupitia (OR) TAMISEMI, kupungua kwa ufunguaji wa kesi katika Mahkama ya Ardhi pamoja na kutokusomeka kwa mapato yatokanayo na Miradi ya Kondominio kwa upande wa Pemba na kusomeka moja kwa moja katika hesabu za Wizara Unguja.

46. **Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 1,283,464,200 (TZS Milioni 444,138,200** Mishahara na **TZS Milioni 839,326,000** Matumizi ya Kawaida).

47. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Miezi Tisa, Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 1,070,765,730 (TZS Milioni 333,103,650** Mishahara na **TZS Milioni 737,662,080** Matumizi ya Kawaida).

48. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi 2026, fedha zilizotumika ni **TZS Milioni 691,368,960.5 (TZS Milioni 342,338,023.5** Mishahara na **TZS Milioni 349,030,937** Matumizi ya Kawaida) sawa na **asilimia 64.6** ya fedha zilizopangwa kwa Miezi Tisa na **asilimia 53.9** kwa Mwaka.

49. **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu ya Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba itaendelea kuratibu shughuli za Wizara Pemba; itaimarisha usimamizi wa masuala ya Kondominio, itaimarisha kazi na usimamizi wa Mipango, Bajeti, na Ufuatiliaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa upande wa Pemba, itaimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi, itawapatia mafunzo ya muda mfupi Wafanyakazi 15, mafunzo ya muda mrefu Wafanyakazi 05 na itasimamia ajira mpya kwa Wafanyakazi 28.

50. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu ndogo ya uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 38,010,000** kutokana na Ada ya Mahkama na Usajili wa Miradi ya Kondominio.

51. **Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 1,517,324,000** ambapo **TZS Milioni 600,024,000** Mishahara na **TZS Milioni 917,300,000** Kazi za Kawaida.

52. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu Kuu PN0201 ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 38,010,000** kutokana na Ada ya Mahkama na Usajili wa Miradi ya Kondominio.

53. **Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Programu Kuu PN0201 ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 4,782,810,000** ambapo **TZS Bilioni 2,320,600,000** Mishahara kwa Idara ya Mipango,

Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi na Afisi Kuu Pemba, **TZS Bilioni 2,462,210,000** kwa Kazi za Kawaida.

**PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI**

**54.** **Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu PN0202 ya Usimamizi wa Ardhi ina jukumu la kuhakikisha usalama na umiliki wa matumizi ya ardhi Nchini, Programu hii ina Programu ndogo moja, ambapo kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, ilikadiriwa kukusanya **TZS Bilioni 10,699,108,136** ambapo **TZS Milioni 535,000,000** zilipangwa kukusanywa kupitia fungu la Wizara na **TZS Bilioni 10,164,108,136** zilipangwa kukusanywa na Kamisheni ya Ardhi.

**55.** **Mheshimiwa Spika;** kwa kipindi cha Miezi Tisa Wizara ilipangiwa kukusanya TZS **Bilioni 7,990,058,615** ambapo **TZS Milioni 415,250,000** kutokana na mapato ya Fungu la Wizara na **TZS Bilioni 7,574,808,615** kwa Kamisheni ya Ardhi.

**56.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya **TZS Bilioni 6,331,667,890** zimekusanywa sawa na **asilimia 79** kwa makadirio ya kipindi cha Miezi Tisa na **asilimia 59** kwa mwaka **(TZS Milioni 245,834,968** zimekusanywa kwa fungu la Wizara sawa na **asilimia 59.4** kwa Miezi Tisa na **asilimia 46.0** kwa mwaka na **TZS Bilioni 6,085,832,922** zimekusanywa na Kamisheni ya Ardhi sawa na **asilimia 80** kwa kipindi cha Miezi Tisa na **asilimia 60** kwa mwaka).

**57.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu Kuu PN0202 ya Usimamizi wa Ardhi iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 4,360,699,200 (TZS Milioni 387,999,200** Mishahara ya Mahakama ya Ardhi, **TZS Bilioni 3,065,000,000** Ruzuku ya Mishahara ya Kamisheni ya Ardhi, TZS **Milioni 507,700,000** Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida ya Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali na **TZS Milioni 400,000,000** kwa Matumizi ya Kawaida ya Mahakama ya Ardhi).

**58.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha miezi Tisa Programu hii iliidhinishiwa kutumia **TZS Bilioni 3,118,329,850 (TZS Milioni 288,179,850** Mishahara ya Mahakama ya Ardhi, **TZS Bilioni 2,298,750,000** Ruzuku ya Mishahara ya Kamisheni ya Ardhi, **TZS Milioni 384,000,000** ni Ruzuku Matumizi ya Kawaida ya Ofisi ya

Mthamini Mkuu wa Serikali na **TZS Milioni 147,400,000** kwa Matumizi ya Kawaida ya Mahakama ya Ardhi).

**59.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, fedha zilizopatikana ni **TZS Bilioni 2,807,420,433.32** ambapo **TZS Bilioni 2,577,119,475** Mishahara **(TZS Milioni 299,008,962.5** Mishahara ya Mahakama ya Ardhi, **TZS Bilioni 2,278,110,512.5** Ruzuku ya Mishahara ya Kamisheni ya Ardhi), **TZS Milioni 78,465,958.32** Matumizi ya Kawaida ya Mahakama ya Ardhi na **TZS Milioni 151,835,000** ni Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida ya Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali) sawa na **asilimia 90.9** kwa Miezi Tisa na **asilimia 68.1** kwa mwaka.

**PROGRAMU NDOGO SN020201: USIMAMIZI WA ARDHI**

**60.** **Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi inatekelezwa na Taasisi Tatu (3) za Wizara ambazo ni Mahkama ya Ardhi, Kamisheni ya Ardhi na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi ilitekeleza shughuli zinazohusiana na masuala ya Ardhi kupitia Taasisi zake kama ifuatavyo:-

**HN02020108: UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI**

**61.** **Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi kupitia Huduma hii inatekelezwa kupitia Mahkama ya Ardhi. Huduma imepewa jukumu la kupokea, kusikiliza na kuyatolea uamuzi mashauri yanayotokana na Migogoro ya Ardhi yanayowasilishwa na Wananchi.

**62.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, Mahkama imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imepokea kesi mpya Mia Moja na Hamsini na Tano (155) ambazo zimefunguliwa Unguja na Pemba. Aidha, Mahakama ya Ardhi imeendelea kusikiliza kesi hizo pamoja na za awali ambapo kesi Mia Moja na Thalathini (130) zimetolewa uamuzi, sawa na wastani wa asilimia 57% ya lengo la kuamua kesi 230 kwa kipindi cha miezi tisa na asilimia (37) ya kesi (350) zilizopangwa kwa mwaka. **Kiambatanisho nambari 4 Kinafafanua.**

ii. Imetoa elimu kwa jamii katika Mikoa yote ya Unguja kupitia ushiriki wa Legal Aids Campaign kwa mashirikiano makubwa na Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Pia, Mahakama ya Ardhi imeendelea kutoa elimu kwa jamii katika Mikoa mitatu ya Unguja kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto katika Wiki ya kupinga udhalilishaji na ukatili wa kijinsi. Mahakama ya Ardhi waliweza kupata fursa ya utoaji wa elimu juu ya kuepuka migogoro ya ardhi na kutoa ufafanuzi juu ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa njia ya Usuluhishi ikiwa ni njia ya amani.

iii. Imetoa elimu kwa njia ya Televisheni (ZBC), kuhusiana na utekelezaji wa Hukumu katika migogoro ya Ardhi.

iv. Imelipa Stahiki kwa Wafanyakazi Ishirini na Mbili (22) ambapo wafanyakazi, Kumi na Moja (11) wamelipwa posho la malipo ya saa za ziada, Mfanyakazi Mmoja (01) amepatiwa mafunzo ya muda mrefu na Wafanyakazi Kumi (10) wamepatiwa posho ya likizo.

**63.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Mahkama ya Ardhi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 15,000,000 TZS** na **Milioni 11,250,000** zilitengwa kwa kipindi cha miezi Tisa kupitia chanzo chake cha Ada ya (Kesi za Ardhi na Kodi za Nyumba).

**64.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya **TZS Milioni 6,049,400** zilikusanywa sawa na **asilimia 53.8** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 40.3** kwa mwaka.

**65.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Matumizi Mahkama ya Ardhi ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS Milioni 787,999,200 (TZS Milioni 387,999,200** Mishahara na **TZS 400,000,000** kwa Matumizi ya Kawaida) na Kwa Kipindi cha Miezi Tisa jumla ya **TZS Milioni 435,579,850** ziliidhinishwa **(TZS Milioni 288,179,850** Mishahara na **TZS Milioni 147,400,000.00** Matumizi ya Kawaida).

**66.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 377,474,920.8 (TZS Milioni 299,008,962.5** Mishahara na **TZS Milioni 78,465,958.3** Matumizi ya Kawaida) sawa na **asilimia 86.6** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 47.9** kwa mwaka.

67. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Mahakama ya Ardhi kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi itaendelea kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri yanayohusiana na migogoro ya ardhi itakayowasilishwa Mahakamani; itayatolea uamuzi mashauri 200 Unguja na Pemba, itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu migogoro ya ardhi na itaendelea kujenga mazingira bora ya kazi.

68. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Mahakama ya Ardhi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 16,290,000** kutokana na Ada ya Mahkama.

69. **Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Mahakama ya Ardhi kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Milioni 701,650,000** ambapo **TZS Milioni 397,890,000** Mishahara na **TZS Milioni 303,760,000** Matumizi ya Kawaida.

**HN02020107: KUSIMAMIA NA KUIDHINISHA RIPOTI ZA UTHAMINI**

70. **Mheshimiwa Spika;** Huduma hii ipo chini ya Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi na inatekelezwa na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kwa madhumuni ya kuhakikisha usimamizi mzuri wa uthaminishaji wa mali kwa malengo mbalimbali ya Sekta ya Umma, Biashara na Wananchi kwa ujumla. Kazi kuu ya Mthamini Mkuu wa Serikali ni kuthibitisha kazi za uthamini zinazofanywa na Wathamini wa Taasisi za Serikali na Taasisi binafsi.

71. **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Mthamini Mkuu imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imethibitisha ripoti 481 kati ya hizo 20 ni ripoti za uthamini mali kwa ajili mikopo (Morgage Purpose), 155 ripoti za uthamini mali kwa ajili ya thamani (Market Value Determination), 112 ripoti za uthamini mali kwa ajili ya mirathi (Inheritance Purpose), 194 ripoti za uthamini mali kwa ajili ya fidia (Compensation Purpose).

ii. Imeandaa Muongozo wa Uthamini wa Mali na Malipo ya Fidia Zanzibar kwa mwaka 2025 ambao utasaidia kupunguza changamoto za uthamini hasa uthamini wa fidia.

iii. Imefanya uthamini wa Mali (Fixed and non fixed Assets) katika Taasisi za Serikali ili kufahamu thamani za Mali za Taasisi hizo (Book Value Determination) kwa ajili kuweka thamani halisi za Serikali kwenye Asset Register za Msajili wa Hazina ambapo ni muhimu kujua aina, idadi, uchakavu na thamani za soko za mali kwa kipindi maalum zinazomilikiwa na Taasisi za umma Nchini.

iv. Imetoa elimu ya Uthamini kwa wadau kupitia Mikutano na Vyombo vya habari kuhusu masuala ya Uthamini ikiwemo umuhimu wa uthaminishaji Mali kwa malengo tofauti hasa katika uthamini wa Fidia, Uthamini kwa ajili ya pango, Uthamini kwa ajili ya Mikopo ya Benki na Uthamini kwa ajili ya Mirathi.

**72.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu hii kupitia Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 520,000,000** na **TZS Milioni 404,000,000** ilikadiriwa kwa kipindi cha Miezi Tisa kutokana na chanzo chake cha mapato ya Ada ya Uthamini.

**73.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya **TZS Milioni 239,785,568** zilikusanywa sawa na **asilimia 59.4** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 46.1** ya makadirio kwa mwaka.

**74.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Matumizi, Ofisi ilipangiwa kutumia Ruzuku ya matumizi ya kawaida ya **TZS Milioni 507,700,000** kwa mwaka na **TZS Milioni 384,000,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa.

**75.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, fedha zilizopatikana ni **TZS Milioni 151,835,000** sawa na a**silimia 61.2** ya makadirio ya Fedha zilizopangwa kwa Miezi Tisa na **asilimia 31** kwa mwaka.

**76.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi itahakiki na kuidhinisha ripoti 650 za uthamini wa rasilimali; itaendelea kusajili na kuwapatia leseni Wathamini 80, Kusambaza na kutoa elimu juu ya Muongozo wa Uthamini wa Mali na Malipo ya Fidia, itatoa elimu ya Uthamini kwa Wadau mbalimbali wenye uhitaji wa uthamini wa fidia

kupitia Vyombo vya habari pamoja na Mikutano kwa Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi, Ofisi itaendelea kuweka kumbukumbu za ripoti za uthamini wa mali zilizofanyiwa Uthamini katika Mfumo na itakamilisha marekebisho ya Sheria ya Ofisi ya Mthamini Mkuu na Bodi ya Usajili wa Wathamini Zanzibar kwa kuzipeleka katika vyombo vya maamuzi sambamba na kuandaa Mfumo wa usajili wa wathamini.

77. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi chini ya huduma ya Kusimamia na Kuidhinisha Ripoti za Uthamini imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 564,720,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

78. **Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi chini ya huduma ya Kusimamia na Kuidhinisha Ripoti za Uthamini iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa Fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako kuidhinisha Ruzuku ya matumizi ya kawaida ya **TZS Milioni 809,270,000** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida.

**HN02020101: UPANGAJI NA USIMAMIZI WA ARDHI**

79. **Mheshimiwa Spika;** Huduma hii ya Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi inatekelezwa na Kamisheni ya Ardhi yenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria za Sekta ya Ardhi na kuziunganisha Idara zote zinazosimamia matumizi na maendeleo ya ardhi. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Huduma imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imesimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mradi wa Kuandaa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi Kisiwani Pemba, Kanuni za Ujenzi za Zanzibar (Building Code) na Mfumo wa Taarifa za Pamoja (Spatial Data Infrastructure) unaoratibiwa na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Programu ya BIG Z.

ii. Imefanya matayarisho ya awali ya utekelezaji wa Mradi wa Mfumo wa Usajili wa Taarifa za Ardhi (LARIS) ikiwemo upatikanaji wa kibali cha kupiga picha za Anga, Utoaji wa Hati katika maeneo yatakayojengwa vituo vya LARIS katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba, kuunda timu za Wataalamu zilizohitajika kwa mujibu wa Mradi na mambo mengine yanayohusu matayarisho ya utekelezaji.

iii. Imepanga jumla ya Miji mitatu (03) (Unguja (1) na Pemba (2) ambao Mji wa Tunguu "Roundabout", Mvumoni na Ukanda wa Pwani wa Kisiwa cha Pemba. Vile vile, Shehia nane (8) za Bambi, Umbuji, Pagali, Jendele, Chwaka, Uroa, Marumbi na Pongwe zimeanza kupangwa kwa ajili ya uhifadhi wa Misitu ya Asili ili kuzuia uvamizi. Pia, Shehia tatu za Kiwengwa, Mkokotoni na Matemwe zimepangwa kwa ajili ya utunzaji wa vyanzo vya maji. Pia, kwa upande wa Mkoa wa Mjini Magharibi Kamisheni imepanga eneo la Kikwajuni kwa Mjerumani kwa ajili ya Mradi wa Mji Mpya wa Nyumba za Makaazi na Biashara. Aidha, kwa upande wa Wilaya ya Kaskazini "B" Shehia tatu (3) zinaendelea na upangaji nazo ni Bumbwini Makoba, Bumbwini Mafufuni na Kiongwe.

iv. Inaendelea na uandaaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi wa Pemba (Pemba Spatial Development Structure Plan) pamoja na upangaji wa maeneo yaliyoendelezwa bila ya mpango ikiwemo eneo la Maungani kwa ajili ya kuimarisha maeneo kwa kuweka njia na huduma za kijamii.

v. Imetambua na kupanga jumla ya viwanja (Parcel) 1,095 kwa ajili ya Makaazi, Biashara, huduma za jamii, maeneo ya wazi pamoja na maeneo ya hifadhi ya vyanzo vya maji.

vi. Imeandaa jumla ya Miongozo ya matumizi ya ardhi (Guidelines) 2,159 (Unguja 1,794 na Pemba 365), kufanya ukaguzi na kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kua na Mipango bora ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya uwekezaji Maziwa Ngombe Micheweni na Fumba kwa Unguja.

vii. Kamisheni ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Uchumi wa Buluu imeandaa Muongozo wa Upangaji wa Maeneo ya Ukanda wa Baharini (Guideline for Local Marine Spatial Planning) na kufanya mikutano minne kwa ajili ya kuelimisha jamii juu ya upangaji wa maeneo ya Bahari.

viii. Imepima viwanja 136 (Unguja 101 na Pemba 35) vya Taasisi za Serikali na viwanja 1,600 (Unguja 950 na Pemba 650) vya maombi ya wananchi.

ix. Imetayarisha na kuhifadhi taarifa 09 za kumbukumbu za ukusanyaji wa Vipimo vya kupwa na kujaa kwa maji ya bahari.

x. Imeweka na kuhuisha vianzio 33 (Unguja 17 na Pemba 16) vya upimaji..

xi. Imeandaa na kutayarisha ramani 1,786 za matumizi ya Ardhi (Ramani 1,458 Unguja na 328 Pemba) na nambari za utambulisho maalum kwa ajili ya ramani za maeneo (ZUPIN) 1,296 (864 Unguja na Pemba 432).

xii. Imeandaa na kuhifadhi ripoti za kitaalamu za upimaji wa ardhi 1,060 (757 Unguja na 303 Pemba).

xiii. Imetayarisha hati 1,319 (Unguja 600 na Pemba 719) za haki ya matumizi ya Ardhi na kuhakiki Hati 308 (Unguja 167 na Pemba 141).

xiv. Imetayarisha Mikataba 209 ya Ukodishwaji wa Ardhi (Unguja 190 na Pemba 19) na kufanya Ukaguzi wa maeneo 395 (Unguja 252 na Pemba 143) ya ukodishwaji wa ardhi pamoja na kuhakiki Mikataba 100 ya ukodishaji wa ardhi (Mikataba Unguja 74 na 26 Pemba).

xv. Imetayarisha hati 440 za Mashamba ya Eka tatu na kufanya ukaguzi wa Mashamba ya Eka tatu 655 (Unguja 502 na 153 Pemba).

xvi. Imefanya kazi 777 za uthamini (Unguja 511 na kwa Pemba 266) pamoja na kutambua maeneo (percel) 1,921 (1,738 Unguja na Pemba183).

xvii. Imefanya utambuzi maeneo 620 ya Uhaulishaji (Unguja 430 na 190 Pemba) pamoja na kupokea na kuhakiki Hati 567 (Unguja 450 na Pemba 117).

xviii. Imesajili Hati 287 (157 Unguja na 130 Pemba) pamoja na kusajili maeneo 54 (Unguja 37 na Pemba 17).

xix. Imetoa hati za utambuzi 631 (Unguja 318 na Pemba 313) pamoja na kufanya usajili wa Kadi 711 (Unguja 408 na Pemba 303).

xx. Imeandaa Mifumo Miwili ya TEHAMA (Mfumo wa Uhaulishaji na Mfumo Usajili wa Hati za Matumizi ya Ardhi) pamoja na kufanya

ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma ya Internet ya uhakika.

**80.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi kupitia huduma ya Upangaji na Usimamizi wa Ardhi ilipanga kukusanya **TZS Bilioni 10,164,108,136** kutoka vyanzo vyake vya Mapato, ikiwemo Nyaraka za Ardhi, Upimaji na Ramani, Usajili, Uthamini na Uhaulishaji na **TZS Bilioni 7,574,808,615** ilikadiriwa kukusanywa kwa kipindi cha Miezi Tisa.

**81.** **Mheshimiwa Spika;** hadi kufikia Machi 2026 Programu kupitia Kamisheni ya Ardhi imefanikiwa kukusanya **TZS Bilioni 6,085,832,922/=** sawa na **asilimia 80.00** ya makadirio ya Miezi Tisa na **asilimia 60** kwa mwaka.

**82.** **Mheshimiwa Spika;** aidha, Kamisheni haikufikia lengo la kukusanya **asilimia 100** kutokana na kusita kuyapima na kutoa mikataba ya ukodishwaji wa maeneo ya ukanda wa Bahari kwa upande wa Pemba.

**83.** **Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamisheni ya Ardhi ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 8,147,054,068 {TZS 3,065,000,000** ruzuku ya Mshahara na **TZS 5,082,054,068** ni Matumizi ya kawaida yanayotokana na **asilimia 50** ya makusanyo ya ndani}. Aidha, kwa Kipindi cha Miezi Tisa Kamisheni ya Ardhi ilikadiria kutumia **TZS Bilioni 6,469,757,586** kati ya hizo **TZS Bilioni 4,171,007,586** ni Matumizi ya kawaida yanayotokana na **asilimia 50** ya makusanyo ya ndani na **TZS Bilioni 2,298,750,000** Ruzuku ya Mishahara.

**84.** **Mheshimiwa Spika;** hadi kufikia Machi 2026, fedha zilizopatikana **TZS Billioni 5,586,694,297.50** kati ya hizo **TZS Bilioni 3,308,583,785** ni matumizi ya kawaida kutoka katika asilimia 50 ya makusanyo na TZS **Milioni 2,278,110,512.5** sawa na **asilimia 86** kwa Kipindi cha Miezi Tisa na **asilimia 69** ya mwaka.

**85.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa Fedha 2026/2027 Programu kupitia Huduma ya Upangaji na Usimamizi wa Ardhi itaandaa hati 2,160 (1,800 Unguja na 360 Pemba) za Haki ya Matumizi ya Ardhi, itaandaa na kusimamia Mikataba 530 (450 Unguja na 80 Pemba) ya ukodishwaji wa Ardhi, itafanya mapitio ya Mikataba ya Kodi za Ardhi 230 (150

Unguja na 80 Pemba). itahakiki na kuyasimamia mashamba 600 ya Ardhi ya Eka tatu (300 Unguja na 300 Pemba), itaendelea na zoezi la kuratibu Kampeni maalumu ya Kupima Ardhi ya Eka Tatu kwa Wilaya zote, itafanya uthamini wa Ardhi kwa maeneo 2,400 (2,000 Unguja na 400 Pemba), itafanya utambuzi wa Ardhi katika maeneo 37,000 (20,000 Unguja 17,000 Pemba). itatangaza maeneo mapya 5 (3 Unguja na 2 Pemba).

**86.** **Mheshimiwa Mwenyeketi;** Pia, itaanzisha mifumo 02 (01Unguja na 01 Pemba) shirikishi ya matumizi ya taarifa za upimaji Ardhi na ramani, itapanga na kupimwa maeneo 2,100 (1,500 Unguja na 600 Pemba) na kuwekewa mipaka kutokana na maombi ya Wananchi, maeneo 425 maombi ya Taasisi na maeneo ya mpango ya Serikali (305 Unguja na 120 Pemba). itahuisha ramani za msingi 12 (10 Unguja na 02 Pemba), itakusanya na kudhibiti taarifa za upimaji wa maeneo ya Ardhi na baharini, pamoja na kusimamia alama msingi za Upimaji, itatayarisha nambari 2,160 (1,800 Unguja na 360 Pemba) za ZUPIN.

**87.** **Mheshimiwa Mwenyekiti:** Pia, itapanga, kuimarisha na kusimamia Miji midogo 6 (4 Unguja na 2 Pemba) pamoja na kuandaa Mipango ya Uimarishaji na Uendeleezaji wa Miji, Jumla ya Mipango 05 ya Maendeleo kwa Vijiji (03 Unguja na 02 Pemba) itapangwa ambavyo vipo karibu na EPZ, Kutangaza katika Gazeti la Serikali na kupangiwa matumizi maeneo 04 (02 Unguja na 02 Pemba) ya Ardhi ya Akiba (land bank). Uroa, Marumbi na Pongwe. Aidha, jumla ya Mipango 05 (03 Unguja na 02 Pemba) ya Uhifadhi pamoja na Mipango ya Kina ya Maneneo ya Ardhi za Akiba itakayoandaliwa. Jumla ya Mipango 02 ya eneo maalum la uhifadhi wa msitu kwa shehia nane Bambi, Pangali, Umbuji, Jendele, Chwaka, Uroa, Matumbi na Pongwe.

**88.** **Mheshimiwa Spika;** itasajili maeneo 3,000 (2,000 Unguja na 1,000 Pemba) yaliyokamilisha vigezo vya usajili pamoja na kutoa kadi 2,300 (1,500 Unguja na 800 Pemba) za usajili wa Ardhi. Vilevile itasajili nyaraka 3,000 (2,000 Unguja na 1,000 Pemba) za maeneo ya utambuzi yaliyosajiliwa. itaratibu vikao 06 (04 Unguja na 02 Pemba) vya wadau maalumu (Taasisi za kifedha, Afisi ya Mufti, Wakfu na Mali ya Amana, BPRA).

89. **Mheshimiwa Spika;** itaandaa Mipango ya muda mfupi, kati na mrefu na Bajeti, aidha, itasimamia utekelezaji wa Miradi. Itaratibu uandaaji wa tafiti 3 (02 Unguja na 01 Pemba) zinazohusiana na masuala ya Ardhi. itaratibu na kufanya vikao 05 vya Bodi ya Utendaji na Usimamizi wa Kamisheni ya Ardhi.

90. **Mheshimiwa Spika;** Kamisheni itaandaa Mikutano 32 (26 Unguja na 06 Pemba) ya kijamii juu uhamasishaji wa masuala ya Ardhi kupitia Kliniki ya Ardhi pamoja na kuelimisha jamii kupitia vyombo vya Habari, Kuandaa kupitia mikutano 08 (04 Unguja na 04 Pemba) kwa jamii juu ya upangaji na usimamizi wa miji, itatoa elimu ya usajili wa Ardhi kupitia Programu 48 (24 Unguja na 24 Pemba) kwa Wananchi pamoja uhamasishaji wa uchukuaji wa hati na kadi. Itaratibu utekelezaji wa Wiki ya Ardhi.

91. **Mheshimiwa Spika;** Kamisheni itaendelea kufanya marekebisho ya sheria 07 za Kamisheni ya Ardhi pamoja na kuandaa mikataba 12 (08 Unguja na 04 Pemba) ya Kisheria ya Kamisheni ya Ardhi. Aidha, kuratibu usalama wa mtandao na ulinzi wa taarifa, kuweka na kusimamia miundombinu imara na yakuaminika (Mtandao wa LAN, WAN na WIFI. itaimarisha na kusimamia mabadiliko katika mageuzi ya kimfumo.

92. **Mheshimiwa Spika;** Kamisheni itaimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwapatia Wafanyakazi stahiki zao, Kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kuipatia Ofisi huduma na vifaa vya kisasa. itaratibu semina 10 za ndani na mambo mtambuka. (4 Unguja na 4 Pemba. itawajengea uwezo wa kitaalamu watendaji 11 katika fani maalumu za Ardhi zikiwemo Hydrographic survey kwa muda mrefu na muda mfupi 48

93. **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi kupitia Huduma ya Upangaji na Usimamizi wa Ardhi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 11,250,200,000** kutoka vyanzo vya mapato.

94. **Mheshimiwa Spika;** ili kuiwezesha, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi kupitia Huduma ya Upangaji na Usimamizi wa Ardhi naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya **TZS Bilioni 8,792,502,428** kati ya hizo **TZS Bilioni 3,167,402,428** ni Mshahara na **TZS Bilioni 5,625,100,000** ni matumizi yanayotokana na **asilimia 50** ya makusanyo

ya mapato ya Kamisheni ya Ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake za kawaida.

95. **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu Kuu PN0202 ya Usimamizi wa Ardhi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 11,831,210,000** kutoka vyanzo vya mapato vitokanavyo na Fungu la Wizara na Fungu la Kamisheni ya Ardhi **(TZS 581,010,000** yanatokana na fungu la Wizara na **TZS 11,250,200,000** yanatokana na Fungu la Kamisheni ya Ardhi).

96. **Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Programu Kuu PN0202 ya Usimamizi wa Ardhi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 10,303,422,428 {TZS Billioni 3,167,402,428** ni Mshahara kwa Kamisheni ya Ardhi, **TZS Milioni 397,890,000** Mshahara ya Mahakama ya Ardhi, **TZS Milioni 303,760,000** Matumizi ya Kazi za Kawaida ya Mahakama ya Ardhi na **TZS Milioni 809,270,000** Ruzuku ya Matumizi ya Kazi za Kawaida ya Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali na **TZS Bilioni 5,625,100,000** ni matumizi yanayotokana na **asilimia 50** ya makusanyo ya mapato ya Kamisheni ya Ardhi kwaajili ya utekelezaji wa kazi zake za kawaida}.

**PROGRAMU KUU PN0203: MAENDELEO YA MAKAAZI**

97. **Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu PN0203 ya Maendeleo ya Makaazi ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa makaazi bora, salama, jumuishi na endelevu kwa wananchi pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa Wawekezaji wa Sekta ya Umma na Binafsi katika huduma ya Makaazi.

98. **Mheshimiwa Spika;** Programu hii kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, ilikadiriwa kukusanya **TZS Bilioni 4,354,000,000** kwa mwaka na **TZS Bilioni 3,265,500,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa.

99. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, **TZS Milioni 627,123,368** zilikusanywa sawa na **asilimia 19.2** kwa Miezi Tisa na **asilimia 14.4** kwa Mwaka. Kupungua kwa makusanyo kutokana na thamani ndogo ya miradi iliyosajiliwa.

100. **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu Kuu PN0203 ya Maendeleo ya Makaazi iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS Bilioni 301,159,296,200 (TZS Milioni 200,832,200** Mishahara ya Idara ya Maendeleo ya Makaazi, **TZS Milioni 838,464,000** Matumizi ya Kazi za Kawaida za Idara ya Maendeleo ya Makaazi na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba na **TZS Bilioni 300,120,000,000** kazi za Maendeleo).

101. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha miezi Tisa Programu iliidhinishiwa kutumia **TZS Bilioni 258,059,385,395 (TZS 150,624,150** Mishahara ya Idara, **TZS 725,636,500** Matumizi ya Kazi za Kawaida ya Idara na Bodi na **TZS 257,183,124,745** Kazi za Maendeleo).

102. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, fedha zilizopatikana ni **TZS Millioni 352,642,735.5 (TZS Milioni 126,744,552** Mishahara, **TZS Milioni 225,898,210.5** Matumizi ya Kazi za Kawaida na hakuna fedha zilizoingizwa kwa Kazi za Maendeleo) sawa na **asilimia 0.14** makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 0.12** kwa mwaka.

103. **Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu PN0203 inatekelezwa kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya za Kondominio na Huduma ya Utatuzi wa Migogoro kwa Wapangaji wa Nyumba. Aidha, Programu hii ina Programu ndogo moja SN020301 ya Maendeleo ya Makaazi.

**PROGRAMU NDOGO SN020301: MAENDELEO YA MAKAAZI**

**HUDUMA HN02030102: USAJILI WA MAJENGO NA JUMUIYA ZA KONDOMINIO.**

104. **Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo ya SN020301 kupitia huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya za Kondominio inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Makaazi ambayo ina jukumu la kusimamia Maendeleo ya Makaazi, kusajili Majengo ya Kondominio, kuratibu upatikanaji wa Makaazi bora na nafuu kwa Wananchi pamoja na kusimamia matumizi ya pamoja kwa majengo yenye sehemu zinazomilikiwa na mtu zaidi ya mmoja. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu ndogo kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya za Kondominio imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imetoa jumla ya fomu Mia Mbili Sabini na Nne (274) kwa Unguja na Pemba za maombi ya usajili wa Kondominio ambapo fomu 158 zilijazwa, zilikidhi vigezo, zilisajiliwa na kutolewa Hati.

ii. Imesajili Ramani Nane (08) za Miradi ya Kondominio ambayo ni AMG Company limited uliopo Michamvi, The System Design Solutions (Phase 3) uliopo Mbweni, TMA Holdings Company limited uliopo Nungwi JNB Zanzibar Limited uliopo Kiwengwa, Sharban Jusab Tharia uliopo Mkunazini, HM Camaradas (Spectral Invest Limited as Developer) uliopo Paje, Itaset Company limited (Yako Hospitality Limited as Developer) uliopo Kiwengwa na Legendary Zanzibar Beach Resort limited uliopo Michamvi.

iii. Imesajili Majengo/Miradi Sita (6) ya Kondominio ambayo ni TMA Holdings Company Limited uliopo Nungwi, Mwerevu Company Limited uliopo Michamvi, Sharban Jusab Tharia uliopo Mkunazini, Johari developers limited uliopo Kizimkazi, System Design Solutions Company Limited (phase 3) uliopo Mbweni na Furaha Investment limited uliopo Bwejuu.

iv. Imesajili Umiliki wa Sehemu/fleti (Unit Registration) Mia Moja Arobaini na Nne (144) za Nyumba za Kondominio katika maeneo ya Michenzani, Kilimani, Mapinduzi, Machomane, Mbuyuni, Madungu, Paje, Jambiani, Mbweni, Malindi, Uroa, Kiwengwa, Kikwajuni, M/kwerekwe na Kwahani.

v. Imefanya ukaguzi wa Miradi ya Kondominio Ishirini (20) kwa lengo la kujiridhisha na kuhakiki michoro na nyaraka zilizo wasilishwa. **Kiambatanisho nambari 5 kinafafanua.**

vi. Imeendelea kufanya uchambuzi na uhakiki wa maombi ya usajili wa fleti Mia Moja Sitini na Moja (161). Uhakiki huu unafanywa kwa kushirikiana na Masheha wa Shehia husika.

vii. Imeendelea na zoezi la utoaji wa elimu kuhusu usajili wa fleti za Kondomonio na uanzishwaji wa Jumuiya za Kondominio kwa Wamiliki na Wakaazi wa Nyumba za Maendeleo pamoja na kutoa elimu kupitia Vyombo vya Habari kwa upande wa Unguja na Masheha 72 kwa Mkoa wa Kusini Pemba.

105. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 4,354,000,000** na **TZS Bilioni 3,265,500,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa.

106. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, Programu imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS Milioni 627,123,368** sawa na **asilimia 19.2** kwa Miezi Tisa na **asilimia 14.4** ya makadirio kwa mwaka.

107. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya ya Kondominio ilipangiwa kutumia **TZS Bilioni 301,077,432,200** kwa ajili ya utekelezaji wa Kazi za Kawaida, Mishahara na Maendeleo **(TZS Milioni 200,832,200** Mishahara, **TZS Milioni 756,600,000** Matumizi ya Kawaida, na **TZS Bilioni 300,120,000,000** Kazi za Maendeleo)

108. **Mheshimiwa Spika;** kwa Kipindi cha Miezi Tisa Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma hii ilipangiwa kutumia **TZS Bilioni 257,994,711,395** ambapo **(TZS Milioni 150,624,150** Mishahara, **TZS Milioni 725,636,500** Matumizi ya kawaida na **TZS Bilioni 257,118,450,745** Kazi za Maendeleo).

109. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026, fedha zilizopatikana ni **TZS Millioni 337,642,735.6 (TZS Milioni 126,744,552** Mishahara, **TZS Milioni 210,898,183.6** Matumizi ya Kazi za Kawaida na hakuna fedha zilizoingizwa kwa Kazi za Maendeleo) sawa na **asilimia 0.13** makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 0.11** kwa mwaka.

110. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo ya Jumuiya ya Kondominio itaendelea kusimamia upatikanaji wa maeneo ya ujenzi wa nyumba, kufanya usajili wa Miradi ya Kondominio 10, Fleti 250 na ramani 10 Unguja na Pemba, itaendelea kuimarisha ushirikiano wa Sekta ya Nyumba Kitaifa; Kikanda na Kimataifa, itatayarisha Miongozo na kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Jumuiya za Kondominio katika maeneo ya pamoja kwa nyumba ambazo zimeshasajiliwa, itaendelea kufanya ukaguzi na uhakiki katika Miradi ya Kondominio, itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na Usajili wa Kondominio, uundaji

wa Jumuiya na Masuala ya Sekta Milki, itasimamia uandaaji wa Sheria ya Sekta Milki Nchini, Kuimarisha na kuweka mazingira mazuri kwa watendaji wa Idara ikiwemo kuwapa uwezo wa kitaaluma, Kuratibu na kusambaza taarifa za sensa ya makaazi kwa wadau tofauti pamoja na kuanzisha Mfumo wa kielektroniki wa Usajili na Kuhifadhi taarifa za Sekta Milki.

**111.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 2,380,980,000** kutokana na Ada ya Usajili wa Kondominio.

**112.** **Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo ya Jumuiya ya Kondominio chini ya Idara ya Maendeleo ya Makaazi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 301,687,320,000/=** kwa kazi za kawaida na Maendeleo ambapo **TZS Milioni 210,170,000/=** Mishahara ya Idara, **TZS Milioni 557,150,000/=** kazi za kawaida na **TZS Bilioni 300,920,000,000/=** kwa Kazi za Maendeleo.

**HN02030105 UTATUZI WA MIGOGORO KWA WAPANGAJI WA NYUMBA.**

**113.** **Mheshimiwa Spika;** Programu ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma ya Utatuzi wa Migogoro kwa Wapangaji wa Nyumba inayotekelezwa na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imeanzishwa kwa Sheria ya kudhibiti kodi za Nyumba, Sura ya 98 ya Mwaka 1953 (Cap. 98 of 1953) kwa lengo la kusikiliza na kuyatolea uamuzi mashauri yanayotokana na migogoro ya upangishaji wa Nyumba za Serikali na Nyumba binafsi. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imetekeleza kazi zifuatazo: -

i. Imepokea mashauri mapya 25 kwa Unguja hivyo kufanya Bodi hii kwa sasa kuwa na Mashauri 35 Unguja na Pemba. Pia, imefanikiwa kusikiliza mashauri Thelathini na Nne (34) Unguja na Pemba na imeyatolea maamuzi mashauri ya Migogoro ya Kodi za Nyumba Kumi (10) kwa Unguja.

ii. Imetoa elimu kwa jamii kuhusu utendaji wa kazi za Bodi kwa Masheha wa Wilaya ya Mjini.

**114.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba ilipangiwa kutumia **TZS Milioni 81,864,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Kazi za Kawaida na **TZS Milioni 64,674,000** ilipangiwa kutumia kwa Kipindi cha Miezi Tisa.

**115.** **Mheshimiwa Spika;** hadi kufikia Machi 2026 Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba ilifanikiwa kutumia **TZS Milioni 15,000,000** sawa na **asilimia 23.2** ya makadirio ya Miezi Tisa na **asilimia 18.3** kwa mwaka.

**116.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma ya utatuzi wa Migogoro ya Nyumba inayotekelezwa na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba itatoa elimu kwa Taasisi za Serikali na jamii kuhusiana na shughuli na majukumu ya kisheria ya Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba Zanzibar na itaongeza ufanisi katika utoaji wa maamuzi ya kesi zinazohusiana na migogoro ya kodi za nyumba kwa kuzitolea maamuzi mashauri Ishirini na Tano (25) Unguja na Pemba.

**117.** **Mheshimiwa Spika;** Ili kuiwezesha Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya Kawaida **TZS Milioni 76,660,000** kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

## SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR

**118.** **Mheshimiwa Spika;** Shirika la Nyumba Zanzibar ni Taasisi inayojitegemea iliyoanzishwa kwa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2014. Taasisi hii imepewa Mamlaka ya kusimamia na kuendeleza Sekta ya Nyumba Zanzibar kwa kuchangia katika ukuaji wa uchumi na Maendeleo ya Makaazi kwa Wananchi wa Zanzibar ili kwenda sambamba na mahitaji ya nyumba kutokana na ongezeko la watu pamoja na utoaji wa huduma za ujenzi na ushauri elekezi. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Shirika la Nyumba imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Limekamilisha na kuzinduwa ujenzi wa Jengo la Makaazi na Biashara Kiembe Samaki ambao ujenzi huo umefanywa na KMKM na kusimamiwa na Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA). Mradi huo unajumuisha nyumba 22 za Makaazi na Eneo la Biashara.

ii. Limekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Shirika Pemba na tayari Ofisi imeshahamiwa. Kazi hiyo ilifanywa na Shirika na kusimamiwa na Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA).

iii. Linaendelea na ujenzi wa majengo 30 yanayojumuisha nyumba 548 za Makaazi na Biashara Kisakasaka ”B” ambapo hatua iliyopo ni kuchimba na kujenga misingi. Aidha, mradi umefikia asilimia 13 ya utekelezaji wake. Mkandarasi wa ujenzi huo ni Crossword Construction Co. Limited na kusimamiwa na Mhandisi Consultant limited.

iv. Linaendelea na ujenzi wa Nyumba za Makaazi Mombasa – kwa Mchina awamu ya pili, kwa sasa lipo katika hatua ya uwekaji wa miundombinu ya maji taka na maji safi, taizi, kufanya ‘skimming’ na kufanya ‘fitting’ za umeme. Aidha, Mradi huo unajengwa na Kampuni ya Emirates Construction limited na kusimamiwa na Shirika la Nyumba na unatarajiwa kukamilika Mei 2026.

v. Linaendelea na Ujenzi wa nyumba 312 za Makaazi na Biashara Kisakasaka” D” ambapo hatua iliyopo, kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi za Mkandarasi na Mshauri Elekezi, kujaza kwa kifusi kwenye misingi pamoja na kuanza kunyanyua nguzo kwenye misingi hiyo. Aidha, Ujenzi huo unatarajiwa kukamilika Mwezi Mei 2027 na Mkandarasi wa ujenzi huo ni Emirates Company na Mshauri elekezi ni Mhandisi Consultant Limited.

vi. Limeanza ujenzi wa jengo la Biashara Maisara (Twin Tower Golf Club) Unguja ambapo ujenzi upo katika hatua za awali za kufanya ‘Site mobilization’, ujenzi wa Ofisi za Mkandarasi na Mshauri Elekezi pamoja na kusafisha eneo la ujenzi zimekamilika. Mkandarasi wa ujenzi huo ni Mkwawa Construction Limited na Mshauri elekezi ni Alhatmy Designing and Engineering Consultancy.

vii. Ujenzi wa nyumba za Makaazi na Biashara Kikwajuni kwa Mjerumani umekamilisha hatua ya ulipaji wa fidia kwa wamiliki wa nyumba pamoja na wapangaji wa nyumba za Shirika. Aidha, eneo la ujenzi tayari limeshazungushwa uzio. Hatua inayoendelea ni kuyavunja majengo yaliyopo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

viii. Linaendelea na ujenzi wa Mradi wa Nyumba 1,095 awamu ya kwanza Chumbuni ambapo kazi zinazoendelea ni ujenzi wa majengo 8 kati ya 22 ikiwa majengo 4 yameshasimama na yanaendelea na kazi za ndani zikiwemo kupiga plasta, kuweka miundombinu ya maji safi na maji taka pamoja na kufanya miundombinu ya umeme. Aidha, kwa upande wa majengo 4 yapo katika hatua ya kujengwa "ground floor". Mkandarasi wa ujenzi huu ni Weihai Huatan Company Limited na Mshauri Elekezi ni NEO Consultant.

ix. Ujenzi wa Nyumba za Makaazi Saateni upo katika hatua za awali za Michoro ya usanifu na makisio ya gharama za ujenzi pamoja na uchunguzi wa udongo (soil test) na Uchunguzi wa kimazingira (Environmental and Social Impact Assessment) zimekamilika.

x. Imeanza ujenzi wa Mradi wa nyumba za Makaazi na Biashara Mabaoni Chakechake hatua za awali za Michoro ya usanifu na makisio ya gharama za ujenzi pamoja na uchunguzi wa udongo (soil test) na Uchunguzi wa kimazingira zimekamilika.

xi. Ujenzi wa jengo la Mkungu Malofa (Mabatini) awamu ya pili unaendelea hatua iliyofikiwa ni kufanya fitting katika 'slab' ya ghorofa ya kwanza, kufanya fitting katika kuta za "ground floor" pamoja na kupiga plasta katika eneo la 'Basement'.

xii. Limefanyia matengenezo nyumba 44 (Unguja nyumba 23 na Pemba Nyumba 21). Aidha, Shirika limefanya ukaguzi wa nyumba 280 za Shirika la Nyumba kwa lengo la kuwatambua wamiliki halali wa Nyumba za Shirika pamoja na kufanya ukaguzi wa matengenezo madogo madogo kufanyika kwenye nyumba za shirika ikiwemo Unguja 30 na Pemba 26.

xiii. Kuendelea na kuuza Mikataba ya ukodishwaji ambapo kwa kipindi cha miezi tisa Julai – Machi jumla ya Mikataba 376 imefanikiwa kutolewa kwa Wapangaji wa nyumba za Shirika (Unguja 272 na Pemba 104.)

xiv. Kuendelea kutoa taarifa na Elimu kwa jamii kuhusu Shirika kupitia Mikutano ya Wananchi na Taasisi za Serikali na Binafsi, Mitandao ya Kijamii na Vyombo vya habari ikiwemo ikiwemo ZBC redio na Televishenina ZHC connect.

Vilevile, Shirika limefanikiwa kutoa Jarida la Kwanza la Shirika la Nyumba Zanzibar lijulikanalo kama "Makaazi Bora Zanzibar". Lengo kuu la jarida hilo ni kulitangaza Shirika na miradi yake ya nyumba za kisasa inayotekelezwa chini ya ZHC. Shirika limejibu na kuyapatia ufumbuzi malalamiko 9 kupitia Programu ya Sema na Rais (SNR).

xv. Limewajengea uwezo Wafanyakazi 40 wa Shirika (Unguja na Pemba) wa fani tofauti kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi kati ya hao wanawake 12 na wanaume 28 pamoja na Wafanyakazi 12 (Unguja 11 na Pemba 1) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Astashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili wakiwemo wanawake 5 na wanaume 7), Wafanyakazi 26 (Unguja 20 na Pemba 6) wamepatiwa stahiki zao za likizo kwa kipindi cha miezi tisa na kutoa huduma za kiofisi kwa **asilimia 100.**

**119.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/26, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Shirika la Nyumba Zanzibar ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 37,536,000,000** kutokana na vyanzo vyake mbali mbali vya mapato (Mauzo ya Nyumba, ruzuku kutoka Serikalini, Mkopo, Kodi, Mikataba, Dhamana, Tozo na ikiwemo huduma ya ujenzi pamoja na huduma ya ushauri elekezi) na kwa kipindi cha Miezi Tisa Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 35,354,250,000.**

**120.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026 Shirika limefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 23,943,065,751** sawa na **asilimia 67.7** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 63.7** ya makario ya mwaka.

**121.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/26, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Shirika la Nyumba imekadiria kutumia jumla ya **TZS Bilioni 34,072,921,390** na **TZS Bilioni 33,318,738,100** kwa kipindi cha Miezi Tisa zilitengwa kwa ajili ya malipo ya Mishahara, Uendeshaji wa Ofisi pamoja na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

ambayo ni ujenzi wa nyumba mpya za makaazi na biashara na baadhi ya matengenezo ya nyumba za Shirika.

**122.** **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2026 Shirika limetumia jumla ya **TZS Bilioni 37,460,771,196** sawa na **asilimia 112** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 110** kwa makadirio ya matumizi yaliyopangwa kwa mwaka. Kuongezeka kwa asilimia hii kumesababishwa na kupatikana kwa fedha za Miradi ya Maendeleo.

**123.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Shirika la Nyumba kupitia Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi itaendelea na Miradi ya ujenzi wa nyumba 3,599 za Makaazi na Biashara katika maeneo ya mbali mbali Unguja na Pemba, kuendelea kuzitunza na kuzifanyia matengenezo nyumba za Shirika Kuongeza juhudi katika kukusanya mapato ya Shirika, Kupanga mipango ya Shirika, pamoja na kusimamia utekelezaji wa kazi zake. Kutoa elimu kwa jamii kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Shirika, Kuimarisha utendaji kazi wa Shirika kwa kutumia Mifumo ya TEHAMA na Kuweka mazingira Bora ya kazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi

**124.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu kupitia Shirika la Nyumba inatarajia kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 303,690,000,000** kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato yakiwemo makusanyo ya ndani Kodi, Mikataba, Dhamana, Ruzuku kutoka Serikalini, Mauzo ya Nyumba, Mkopo, Tozo pamoja na kazi za Ujenzi na Ushauri Elekezi.

**125.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu kupitia Shirika la Nyumba imekadiria kutumia jumla ya **TZS 301,393,766,695** kwa matumizi ya Mshahara, Uendeshaji wa Ofisi pamoja na matengenezo ya Nyumba za Shirika. **(TZS 1,976,666,195** malipo ya Mishahara, **TZS 4,420,100,500** Gharama za Uendeshaji wa Ofisi, **TZS 294,205,000,000** gharama za utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na biashara na **TZS 792,000,000/=** gharama za matengenezo ya Nyumba za Shirika.

**126.** **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu Kuu PN0203 ya Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS Bilioni 2,380,980,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

127. **Mheshimiwa Spika;** Ili Programu Kuu PN0203 ya Maendeleo ya Makaazi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 301,763,980,000/=** kwa kazi za kawaida na Maendeleo ambapo **TZS Milioni 210,170,000/=** Mishahara, **TZS Milioni 557,150,000/=** kazi za kawaida, **TZS Milioni 79,660,000** ni matumizi ya kazi za kawaida kwa Bodi ya Kodi za Nyumba na **TZS Bilioni 300,920,000,000/=** kazi za Maendeleo.

## VIPAUMBELE VYA BAJETI YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.

128. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imejipanga kutekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kujenga nyumba mpya za Makaazi na Biashara pamoja na kufanya matengenezo ya nyumba zilizopo;

ii. Kuandaa na kufanya mapitio ya Mipango Mikuu na Mipango ya Kina ya Matumizi ya Ardhi Unguja na Pemba;

iii. Kuandaa Mifumo ya TEHAMA ya utoaji wa huduma kwa Jamii katika Sekta ya Ardhi na Makaazi;

iv. Kufanya utambuzi wa maeneo mbalimbali Unguja na Pemba;

v. Kuelimisha Jamii kuhusiana na masuala ya Ardhi na Makaazi kupitia Kliniki ya Ardhi na vyombo vya Habari; na

vi. Kuandaa Miongozo ya Ujenzi ya Nyumba za Makaazi (Building Codes).

## MAOMBI YA IDHINI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.

129. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako liidhinishe Ukusanyaji wa Mapato ya Fedha **TZS Bilioni 3,000,000,000** kutoka vyanzo vilivyomo ndani ya fungu la Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi na Makaazi. **Kiambatanisho namba 6 (a) Kinafafanua.**

130. **Mheshimiwa Spika;** vilevile, naliomba Baraza lako kuidhinisha **TZS Bilioni 11,250,200,000** kutoka vyanzo vilivyomo ndani Fungu la Kamisheni ya Ardhi. **Kiambatanisho namba 6 (b) Kinafafanua.**

131. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, ili Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi iweze kutekeleza Programu Kuu na Programu Ndogo nilizozieleza, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS Bilioni 308,057,710,000** kati ya hizo **TZS Bilioni 7,137,710,000** kwa kazi za Kawaida na Mishahara kwa fungu la Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi **{TZS Bilioni 2,928,660,000** Mishahara ya Idara zilizo chini ya Wizara, **TZS Bilioni 3,399,780,000** Matumizi ya Kawaida ya Idara zilizo chini ya Wizara, T**ZS Milioni 809,270,000** Ruzuku ya Matumizi ya kawaida ya Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali} na **TZS Bilioni 300,920,000,000** kwa kutekeleza Kazi za Maendeleo kwa Fungu la Wizara. **Kiambatanisho namba 6 (c) kinafafanua.**

132. **Mheshimiwa Spika;** Vilevile, naliomba Baraza lako kuidhinisha **TZS Bilioni 8,792,502,428 {TZS Bilioni 3,167,402,428** ikiwa ni Mishahara ya Fungu la Kamisheni ya Ardhi na **TZS Bilioni 5,625,100,000** Ruzuku ya Matumizi ya Kazi za Kawaida yanayotokana na **asilimia 50** ya makusanyo ya Fungu la Kamisheni ya Ardhi. Kiambatanisho namba 6 (d) kinafafanua

**SHUKRANI**

133. **Mheshimiwa Spika;** baada ya uwasilishaji huo sasa nachukua fursa hii kwa mara nyengine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia fursa na uwezo wa kuisoma Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

134. **Mheshimiwa Spika;** vilevile, naomba kumshukuru tena Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa miongozo na maelekezo yake anayotupatia iliyopelekea kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi na kutoa huduma bora kwa Wananchi kupitia Sekta ya Ardhi na Makaazi. Aidha, namshukuru tena Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais kwa maelekezo yake anayotupatia. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa busara, uadilifu, afya njema na maisha marefu pamoja na familia yake.

**135. Mheshimiwa Spika;** kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA na Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati nikisoma Hotuba ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.

**136. Mheshimiwa Spika;** napenda kuwashukuru Wadau wote walioshirikiana nasi kwa njia moja au nyengine wakiwemo Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Washirika wa Maendeleo, Sekta binafsi, Asasi za Kiraia na Jamii kwa Ujumla. Wadau hao ni pamoja Wizara ya Ardhi ya Korea, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala bora, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (SJMT); Wizara ya Fedha na Mipango; Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalamu za SMZ; Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; Wizara Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo; Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Wizara ya Mawasiliano, Teknologia na Ubunifu; Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs); Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA); Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali; Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA); Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Taasisi ya Afisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utendaji kazi wa Serikali (ZPDB).

**137. Mheshimiwa Spika;** vilevile, nawashukuru Ubalozi wa Uingereza, Shirika la Umoja wa Mataifa la Makaazi Duniani (UN – HABITAT), Benki ya Dunia, IGNFI, Kampuni ya Infinity, Zanzibar and WEIHAI, VIGAN STAN, KINGS PRIDE, HOJUNG SOLUTION ya Korea, Benki na Taasisi za Fedha; Masheha pamoja na Wananchi kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia uliochangia kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi.

**138. Mheshimiwa Spika;** Kipekee naomba niushukuru Uongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi hususan Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Mheshimiwa Salha Mohammed Mwinjuma; Katibu Mkuu Ndugu Khadija Khamis Rajab; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Mhaza Gharib Juma; Afisa Mdhamini Ndugu Bakari Ali Bakari; Mkurugenzi Mkuu Shirika la Nyumba Ndugu Sultan Said Suleiman;

Katibu Mtendaji Kamisheni ya Ardhi Ndugu Mussa Kombo Bakari; Wakurugenzi wote, Wakuu wa Taasisi na Wafanyakazi wote kwa kuwa na mimi bega kwa bega katika kuhakikisha Wizara inatekeleza majukumu yake kama ilivyojipangia kulingana na Mipango Mikuu ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa inayohusiana na Sekta ya Ardhi na Makaazi.

139. **Mheshimiwa Spika;** Pia, Navishukuru Vyombo vyote vya habari vilivyoshirikiana nasi katika kuelimisha jamii juu ya shughuli zinazofanywa na Wizara vikiwemo ZBC TV na Redio, TBC, ZCTV, ITV, STAR TV, AZAM TV, CHANNEL 10, TIFU TV, WASAFI, Milard Ayo, Mtegani Redio, Zenj Redio, Zinjibar TV, Zanzibar Leo na Nipashe.

140. **Mheshimiwa Spika;** Vilevile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa familia yangu kwa upendo wao mkubwa, michango yao, uvumilivu, subira na ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu niliyopewa. Aidha, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru kinamama wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa ushirikiano wao wa hali ya juu na kwa kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo.

141. **Mheshimiwa Spika;** shukurani za pekee kabisa ziwaendee Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Unguja na Pemba kwa Ushirikiano wao mkubwa walionipatia kwa kipindi chote ninachohudumia Wizara hii. Namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie wote afya njema na maisha marefu yenye kheri ili waweze kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## HITIMISHO

142. **Mheshimiwa Spika;** nawaomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waipokee, waijadili kwa kina Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, kisha watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe makadirio haya. Tuna imani kubwa kuwa michango ya Waheshimiwa Wajumbe itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha Mwaka wa Fedha 2026/2027.

143. **Mheshimiwa Spika;** naomba kutoa hoja.



…………………………………

**MHESHIMIWA RAHMA KASSIM ALI (MBM),**
**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI,**
**ZANZIBAR.**

# VIAMBATISHO

**KIAMBATANISHO NAMBARI: 1(a) MUHTASARI WA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 - MACHI 2026.**

| TAASISI | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA KWA MWAKA | FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOKUSANYWA JULAI 2025 – MACHI 2026 | ASILIMIA YA FEDHA ILIYOKUSANYWA (KWA MIEZI TISA) | ASILIMIA YA FEDHA ILIYOKUSANYWA (KWA MWAKA) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **AFISI KUU PEMBA** | **1422008** | Ada ya Vibali vya Ujenzi (DCU) | 80,800,000 | 60,600,000 | 920,000 | **1.52%** | **1.14%** |
| | **1422072** | Ada ya Mahakama | 15,000,000 | 11,250,000 | 2,428,400 | **21.59%** | **16.19%** |
| | **1422119** | Ada ya Usajili wa Kondominio | 20,000,000 | 15,000,000 | 0 | **0.00%** | **0.00%** |
| | **Jumla ndogo** | | **115,800,000** | **86,850,000** | **3,348,400** | **3.9%** | **2.9%** |
| **IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI** | **1422008** | Ada ya Vibali vya Ujenzi (DCU) | 2,610,010,000 | 1,957,507,500 | 276,580,700 | **14.1%** | **10.6%** |
| | **Jumla ndogo** | | **2,610,010,000** | **1,957,507,500** | **276,580,700** | **14.1%** | **10.6%** |
| **JUMLA** | | | **2,725,810,000** | **2,044,357,500** | **279,929,100** | **13.7%** | **10.3%** |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAM YA USIMAMIZI WA ARDHI - PN0202** | | | | | | | |
| OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI | **1422093** | Ada ya Uthamini | 520,000,000 | 404,000,000 | 239,785,568.00 | **59.4%** | **46.1%** |
| MAHAKAMA YA ARDHI | **1422072** | Ada ya Mahakama | 15,000,000 | 11,250,000 | 6,049,400.00 | **53.8%** | **40.3%** |
| | **Jumla ndogo** | | **535,000,000** | **415,250,000** | **245,834,968** | **59.20%** | **46.00%** |
| KAMISHENI YA ARDHI | **1422008** | Nyaraka za Ardhi | 1,415,307,241 | **1,025,045,063** | **531,286,113** | **52%** | **38%** |
| | **1422028** | Muongozo wa matumizi ya ardhi | 450,893,124 | **342,776,093** | **212,861,500** | **62%** | **47%** |
| | **1422043** | Ada ya upimaji na ramani | 1,574,240,104 | **1,207,713,531** | **797,065,602** | **66%** | **51%** |
| | **1422072** | Ada ya Usaji wa Ardhi | 130,951,110 | **95,676,833** | **57,323,850** | **60%** | **44%** |
| | **1422093** | Ada ya Uthamini | 135,526,049 | **96,205,112** | **48,407,800** | **50%** | **36%** |
| | **1422090** | Uhaulishaji wa Ardhi | 6,457,190,508 | **4,807,392,884** | **4,438,888,057** | **92%** | **69%** |
| | **Jumla ndogo** | | **10,164,108,136** | **7,574,808,615** | **6,085,832,922** | **80%** | **60%** |
| **JUMLA** | | | **10,699,108,136** | **7,990,058,615** | **6,331,667,890** | **79%** | **59%** |
| **PROGRAM YA MAENDELEO YA MAKAAZI - PN0203** | | | | | | | |
| IDARA YA MAENDELEO YA MAKAAZI | **1422119** | Ada ya Usajili wa Kondominio | 4,354,000,000 | 3,265,500,000 | 627,123,368.00 | **19.2%** | **14.4%** |
| **Jumla ndogo** | | | **4,354,000,000** | 3,265,500,000 | 627,123,368.00 | **19.2%** | **14.4%** |
| **JUMLA KUU** | | | **17,778,918,136** | **13,299,916,115** | **7,238,720,358** | **54.4%** | **40.7%** |

**KIAMBATANISHO NAMBARI 1(b) MUHTASARI WA MATUMIZI YA PROGRAMU KUU NA PROGRAMU NDOGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 – MACHI 2026 IKILINGANISHWA KWA MAKADIRIO YA MWAKA**

| PROGRAMU KUU | IDARA/ TAASISI | MAKISIO KWA MWAKA | MAKISIO KWA ROBO TATU | KILICHOPATIKANA KWA ROBO TATU | MISHAHARA NA POSHO | MATUMIZI MENGINEYO | MATUMIZI YA RUZUKU YA OC | MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO | ASILIMIA YA ROBO 3) | ASILIMIA YA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 36,629,195,200 | 32,719,418,305 | 289,034,656.1 | 143,290,500.0 | 145,744,156.1 | 0.0 | 0 | 0.96% | 0.8% |
| | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 2,053,245,200 | 1,588,122,150.00 | 1,455,480,782.5 | 1,154,390,709.5 | 301,090,073.0 | 0.0 | 0 | 91.7% | 70.9% |
| | Ofisi Kuu Pemba | 1,283,464,200 | 1,070,765,730.00 | 691,368,960.5 | 342,338,023.5 | 349,030,937.0 | 0.0 | 0 | 64.6% | 53.9% |
| | **Jumla ndogo** | **39,965,904,600** | **35,378,306,185.00** | **2,435,884,399.1** | **1,640,019,233.0** | **795,865,166.1** | | **0** | **6.9%** | **6.1%** |
| Usimamizi wa Ardhi | Mahakama ya Ardhi | 787,999,200 | 435,579,850.00 | 377,474,920.8 | 299,008,962.5 | 78,465,958.3 | 0.0 | 0 | 86.6% | 47.9% |
| | Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali | 507,700,000 | 384,000,000.00 | 151,835,000.0 | - | - | 151,835,000 | 0 | 61.2% | 31% |
| | **Jumla ndogo** | **1,295,699,200** | **819,579,850.00** | **529,309,920.8** | **299,008,962.5** | **78,465,958.3** | **151,835,000** | **0** | **77.2%** | **41.2%** |
| | Kamisheni ya Ardhi (Mishahara) | 3,065,000,000 | 2,298,750,000.00 | 2,278,110,512.5 | 2,278,110,512.5 | - | 0.0 | 0 | 90.9% | 68.1% |
| | **Jumla ndogo** | **3,065,000,000** | **2,298,750,000.00** | **2,278,110,512.5** | **2,278,110,512.5** | **0.0** | **0.0** | **0** | **90.9%** | **68.1%** |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **JUMLA** | **4,360,699,200** | **3,118,329,850** | **2,807,420,433.3** | **2,577,119,475.0** | **78,465,958.3** | **151,835,000** | **0** | **90.9%** | **68.10%** |
| Maendeleo ya Makaazi | Idara ya Maendeleo ya Makaazi | 301,077,432,200 | 257,994,711,395.00 | 337,642,735.6 | 126,744,552.0 | 210,898,183.6 | 0.0 | 0 | 0.13% | 0.11% |
| | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba | 81,864,000 | 64,674,000.00 | 15,000,000.0 | - | 15,000,000.0 | 0.0 | 0 | 23.2% | 18.3% |
| | **Jumla ndogo** | **301,159,296,200** | **258,059,385,395** | **352,642,736** | **126,744,552** | **225,898,184** | **0** | **0** | **0.14** | **0.12** |
| | **JUMLA KUU** | **345,485,900,000** | **296,556,021,430** | **5,595,947,568** | **4,343,883,260** | **1,100,229,308** | **151,835,000** | **0.0** | **1.9%** | **1.6%** |

**KIAMBATANISHO NAMBARI 2**

**IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOPATIWA STAHIKI**

| NAM. | AINA YA STAHIKI | WANAUME | WANAWAKE | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | **WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI- UNGUJA** | | | |
| 1. | LIKIZO | 10 | 10 | 20 |
| 2. | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | 7 | - | 7 |
| 3. | WALIOAJIRIWA | - | - | - |
| 4. | UBANI | - | 3 | 3 |
| 5. | PERFORMANCE APPRISAL | 12 | 18 | 30 |
| | **JUMLA** | **29** | **31** | **60** |
| | **KAMISHENI YA ARDHI** | | | |
| 6. | LIKIZO | 17 | 20 | 28 |
| 7. | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | 68 | 41 | 109 |
| 8. | WALIOAJIRIWA | 1 | 1 | 2 |
| 9. | UBANI | 3 | 1 | 4 |
| 10. | PERFORMANCE APPRISAL | 14 | 20 | 34 |
| | **JUMLA** | **287** | **212** | **499** |
| | **MAHKAMA YA ARDHI** | | | |
| 11. | LIKIZO | 4 | 6 | 10 |
| 12. | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | 9 | 2 | 11 |
| 13. | WALIOAJIRIWA | - | - | - |
| 14. | UBANI | 4 | 2 | 6 |
| 15. | PERFORMANCE APPRISAL | 24 | 23 | 47 |
| | **JUMLA** | **40** | **31** | **74** |
| | **MTHAMINI MKUU WA SERIKALI** | | | |
| 16. | LIKIZO | 1 | 2 | 3 |
| 17. | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | - | - | - |
| 18. | WALIOAJIRIWA | - | - | - |
| 19. | UBANI | - | - | - |
| 20. | PERFORMANCE APPRISAL | 12 | 8 | 20 |
| | **JUMLA** | **13** | **10** | **23** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **SHIRIKA LA NYUMBA** | | | |
| 21. | LIKIZO | 11 | 15 | 26 |
| 22. | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | - | - | - |
| 23. | WALIOAJIRIWA | 1 | - | 1 |
| 24. | UBANI | 3 | 4 | 7 |
| 25. | PERFORMANCE APPRISAL | - | - | - |
| | **JUMLA** | **15** | **19** | **34** |
| | **AFISI KUU-PEMBA** | | | |
| 26. | LIKIZO | 3 | 6 | 9 |
| 27. | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | 8 | 8 | 16 |
| 28. | WALIOAJIRIWA | - | - | - |
| 29. | UBANI | - | - | |
| 30. | PERFORMANCE APPRISAL | 9 | 7 | 16 |
| | **JUMLA** | **20** | **21** | **41** |

**KIAMBATANISHO NAMBARI: 3(a)**

**MAFUNZO YA MUDA MFUPI KWA WAFANYAKAZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI**

**KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

| S/N | TAASISI | M'ME | | W'KE | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | NDANI YA NCHI | NJE YA NCHI | NDANI YA NCHI | NJE YA NCHI | |
| 1. | UTUMISHI NA UENDESHAJI | 13 | - | 8 | - | 21 |
| 2. | MIPANGO SERA NA UTAFITI | - | - | - | - | - |
| 3. | IDARA YA MAENDELEO YA MAKAAZI | - | - | - | - | - |
| 4. | MAHAKAMA YA ARDHI | 2 | - | 4 | | 6 |
| 5. | SHIRIKA LA NYUMBA | 28 | - | 12 | - | 40 |
| 6. | MTHAMINI MKUU | 2 | - | 8 | - | 10 |
| 7. | KAMISHENI YA ARDHI | 12 | | 15 | | 27 |
| 8. | OFISI KUU PEMBA | 1 | | 4 | | 5 |
| | **JUMLA KUU** | **58** | | **51** | - | **109** |

## KIAMBATANISHO NAMBARI: 3(b)

### MAFUNZO YA MUDA MREFU KWA WAFANYAKAZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI 2025/2026

| TAASISI | AINA YA MAFUNZO | W'ME | W'KE | JUMLA | CHUO | MWAKA WA KUMALIZA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI** | Masters ya Mipango Miji na Vijiji | 1 | | 1 | University of Jiotong (CHINA) | 2027 |
| **MAHKAMA YA ARDHI** | Degree in Law and Sharia | | 1 | 1 | Zanzibar University(ZU) | 2028 |
| | Master in Human Resource Management | | 1 | 1 | Tanzania Institute of Accountancy (TIA) | 2026 |
| **SHIRIKA LA NYUMBA** | Bachelor Degree in Architecture | | 1 | 1 | Ardhi University | 2028 |
| | Bachelor Degree in Procurement & Supply | 1 | | 1 | Open University | 2026 |
| | Master of Science in Economics and Finance – Project Planning and Management | 1 | | 1 | Zanzibar University | 2026 |
| | Master Program of International Business | 1 | | 1 | Harbin University of Commerce | 2026 |
| | Bachelor Degree of Record and Archives | | 1 | 1 | Utawala wa Umma (IPA) | 2026 |
| | Master in Business Administration | | 1 | 1 | Zanzibar University | 2026 |
| | Master of Business Administration in a Corporate | 1 | | 1 | Institute of Accountancy | 2026 |
| | Master of Project Management | 1 | | 1 | Open University | 2026 |
| | Masters of science in economics and finance - | | 1 | 1 | Zanzibar University | 2026 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Project Planning and Management | | | | | |
| | Master of Human Resource Management with Information Technology | | 1 | 1 | Tanzania Institute of Accountancy | 2026 |
| | Master of procurement and supply | | 1 | 1 | Institute of Accountancy | 2026 |
| | Master of procurement and supply | 1 | | 1 | Institute of Accountancy | 2026 |
| **KAMISHENI YA ARDHI** | | | | | | |
| | Degree in Secretarial Information Management | | 1 | 1 | Kampla Unirvesity-Uganda | 2028 |
| | Masters in Technical In Data Science & Artificial Intelligence | 1 | | 1 | Indian Institute Of Technology Madras-Bweleo Zanzibar | 2025 |
| | Procurement and Logistics Management | | 1 | 1 | Kampala University | 2026 |
| | Degree in Secretarial Information and Office Management | | 1 | 1 | Kampala University | 2026 |
| | Human Resources Management | | 1 | 1 | Institute of Public Adminitration | 2026 |
| | Environment Planning and Management. | | 1 | 1 | Mipango Dodoma | 2027 |
| | Diploma in Computer Science & It, Network | 1 | | 1 | Kampala University-Uganda | 2026 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Bachelor Degree In Science in Real Estate Finance and Investment | 1 | | 1 | Ardhi University-Dar-Es-Salaam | 2028 |
| | Gis and Remote Sensing | | 2 | 2 | University Of Technology Malaysia | 2026/2027 |
| | Master's Program of Urban And Rural Planning | 1 | | 1 | Beijing Jiaotong University-China | 2026 |
| | Master in Science in Economic | 1 | | 1 | ZU | 2027 |
| | Degree in Project Planning and Management | 1 | | 1 | "Institute Of Counting And Professional Studies" Chukwani | 2026 |
| | Geodesy and Geoinformatics (Specialization in Hydography) | 1 | | 1 | Hafencity University -Ujerumani | 2029 |
| | Science in Marine Science specialisation in Marine and Costal Geo-informatics | 1 | | | UDSM | 2028 |
| **OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI** | Masters in Law and Sheria | | | 1 | Kampla Unirvesity-Uganda | 2028 |
| | Degree in Record and Achieves Management | | | 1 | Chuo Cha Utawala Wa Umma (IPA) | 2027 |
| | PhD in Global and Regional Studies | | | 1 | Chuo Kikuu Huria (Out-Zanzibar) | 2027 |
| **OFISI KUU - PEMBA** | Degree in record and Achieve Management | | 1 | 1 | Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) | 2026 |
| | Degree in Secretarial Information Management | | 1 | 1 | Kampla Unirvesity-Uganda | 2026 |
| | Diploma in Law | 1 | | 1 | Zanzibar University(ZU) | 2026 |

**KIMABATISHO NAMBARI: 4**

**KESI ZILIZOPOKELEWA NA KUTOLEWA MAAMUZI KWA KIPINDI CHA KUTOKA JULAI, 2025 HADI MACHI, 2026.**

| S/NO | MKOA HUSIKA | KESI MPYA ZILIZOPOKELEWA | KESI ZILIZOTOLEWA MAAMUZI | KESI ZINAZOENDELEA MAHAKAMANI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mjini Magaharibi | 55 | 35 | 119 |
| 2. | Kaskazini Unguja | 18 | 8 | 46 |
| 3. | Kusini Unguja | 28 | 30 | 50 |
| 4. | Kaskazini Pemba | 22 | 20 | 26 |
| 5. | Kusini Pemba | 32 | 37 | 34 |
| | **JUMLA** | **155** | **130** | **275** |

**KIAMBATANISHO NAMBARI: 5**

**USAJILI NA UKAGUZI WA MIRADI YA KONDOMINIO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.**

| NAMB. | JINA LA MRADI | WILAYA | MAHALI ULIPO |
|---|---|---|---|
| 1. | Said Majid Said (Zahran Abdalla Salum and Seif Said Hemed As Developer) | MJINI | VIKOKOTONI |
| 2. | Zantexas Investment limited | MAGHARIBI 'B' | BWELEO |
| 3. | Abdulkarim Mohammed Abdi and Tofa Saleh Suleiman | MAGHARIBI 'B' | MWANAKWEREKWE |
| 4. | Ballardini Company Limited (Ycona Luxury Resort) | KATI | UROA |
| 5. | Frog Traveler Limited | KASKAZINI 'A' | NUNGWI |
| 6. | Vigor International Company Limited (Johari as Developer) | KASKAZINI 'A' | NUNGWI |
| 7. | Moyo Mzuri Villas Resort Zanzibar Limited | KASKAZINI 'A' | FUKUCHANI |
| 8. | Just Heaven Company Limited | KASKAZINI 'A' | MATEMWE |
| 9. | Itaset Company limited | KASKAZINI 'B' | KIWENGWA |
| 10. | Sea View Property Limited (Lapili Residence),(Breeze Residence), AND (Padel Sporting& Residence) | KASKAZINI 'B' | KIWENGWA |
| 11. | AD Astra Development Limited | KUSINI | PAJE |
| 12. | Mussa Dream Houses | KUSINI | PAJE |
| 13. | Safari Njema Group Limited | KUSINI | PAJE |
| 14. | Zanzibar Villas Limited | KUSINI | PAJE |
| 15. | Sam 2009 Limited | KUSINI | MAKUNDUCHI |
| 16. | Floton Africa Company limited | KUSINI | PAJE |
| 17. | Jambiani Group Company Limited | KUSINI | JAMBIANI |
| 18. | Nyumba za Maendeleo | WETE | MTEMANI |
| 19. | Dimbani Villas & Property Management Company Limited | KUSINI | KIZIMKAZI |
| 20. | Johari Developers Limited | KUSINI | KIZIMKAZI |

**KIAMBATANISHO NAMBARI: 6(a)**

**MAKADIRIO YA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA FUNGU LA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.**

| TAASISI | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA |
|---|---|---|---|
| **PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI - PN0201** | | | |
| | 1422119 | Ada ya usajili wa Kondominio | 21,720,000 |
| | 1422072 | Ada ya Mahakama | 16,290,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **38,010,000** |
| **JUMLA** | | | **38,010,000** |
| **PROGRAMU YA USIMAMIZI WA ARDHI -PN0202** | | | |
| MTHAMINI WA ARDHI | 1422093 | Ada ya Uthamini | 564,720,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **564,720,000** |
| MAHAKAMA YA ARDHI | 1422072 | Ada ya Mahakama | 16,290,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **16,290,000** |
| **JUMLA** | | | **581,010,000** |
| **PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKAAZI – PN0203** | | | |
| IDARA YA MAENDELEO YA MAKAAZI | 1422119 | Ada ya usajili wa Kondominio | 2,380,980,000 |
| | **Jumla ndogo** | | |
| **JUMLA KUU** | | | **3,000,000,000** |

## KIAMBATANISHO NAMBARI: 6(b)

## MAKADIRIO YA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA FUNGU LA KAMISHENI YA ARDHI KWA MWAKA WA FEDHA 202620

| TAASISI | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA |
|---|---|---|---|
| **KAMISHENI YA ARDHI** | 14220157 | NYARAKA ZA ARDHI | 1,280,864,181.00 |
| | 14220258 | MUONGOZO WA MATUMIZI YA ARDHI | 549,370,836.00 |
| | 14220145 | ADA YA UPIMAJI NA RAMANI | 1,574,620,280.00 |
| | 14220157 | USAJILI WA ARDHI | 142,923,612.00 |
| | 14220111 | ADA YA UTHAMINI WA ARDHI | 153,123,612.00 |
| | 14220157 | UHAULISHAJI WA ARDHI | 7,549,297,479.00 |
| | **JUMLA** | | **11,250,200,000.00** |

**KIAMBATANISHO NAMBARI: 6 (c)**

**MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI KWA FUNGU LA WIZARA NA KAMISHENI YA ARDHI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

| Na. | PROGRAMU | PROGRAMU NDOGO | TAASISI/IDARA | MAKISIO KWA MWAKA 26/27 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **MATUMIZI MENGINEYO** | **MISHAHARA/ RUZUKU** | **RUZUKU** | **KAZI ZA MEANDELEO** | **JUMLA YA FEDHA ILIYOPANGWA** |
| 1 | Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | 1. Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 653,282,000 | 269,120,000 | _ | - | **922,402,000** |
| | | 2. Utawala na Uendeshaji | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 891,628,000 | 1,451,456,000 | _ | _ | **2,343,084,000** |
| | | 3. Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | Afisi Kuu Pemba | 917,300,000 | 600,024,000 | _ | _ | **1,517,324,000** |
| | | Jumla ndogo | | **2,462,210,000** | **2,320,600,000** | **_** | **-** | **4,782,810,000** |
| 2 | Usimamizi wa Ardhi | 1. Usimamizi wa Ardhi | Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali | _ | _ | 809,270,000 | _ | **809,270,000** |
| | | | Mahakama ya Ardhi | 303,760,000 | 397,890,000 | _ | _ | **701,650,000** |
| | | **Jumla Ndogo** | | **303,760,000** | **397,890,000** | **809,270,000** | **-** | **1,510,920,000** |
| 3 | Maendeleo ya Makaazi | 1. Maendeleo ya Makaazi | Idara ya Maendeleo ya Makaazi | 557,150,000 | 210,170,000 | _ | 300,920,000,000 | **301,687,320,000** |
| | | | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba | 76,660,000 | _ | _ | _ | **76,660,000** |
| | | | **Jumla ndogo** | **633,810,000** | **210,170,000** | **_** | **300,920,000,000** | **301,763,980,000** |
| | | | **JUMLA KUU** | **3,399,780,000** | **2,928,660,000** | **809,270,000** | **300,920,000,000** | **308,057,710,000** |

**KIAMBATANISHO NAMBARI: 6 (d)**

**MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI KWA FUNGU LA KAMISHENI YA ARDHI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

| NA. | PROGRAMU | PROGRAMU NDOGO | TAASISI/IDARA | MAKISIO KWA MWAKA 26/27 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MATUMIZI MENGINEYO | MISHAHARA/ RUZUKU | RUZUKU | KAZI ZA MEANDELEO | JUMLA YA FEDHA ILIYOPANGWA |
| 1. | Upangaji na Usimamizi wa Ardhi | Utawala na Usimamizi wa Ardhi | Idara ya Ardhi | 546,828,471 | - | _ | - | 546,828,471 |
| | | Upimaji na Utayarishaji wa Ramani | Idara ya Upimaji na Ramani | 549,625,061 | - | _ | _ | 549,625,061 |
| | | Uandaaji wa Mipango wa Matumizi ya Ardhi | Idara ya Mipango Miji na Vijiji | 387,362,767 | - | _ | _ | 387,362,767 |
| | | Usajili wa Ardhi | Afisi ya Msajili wa Ardhi | 239,924,938 | - | - | - | 239,924,938 |
| | | **Jumla ndogo** | | **1,723,735,237** | _ | - | | **1,723,735,237** |
| 2. | Utawala na Uendeshaji wa Kamisheni ya Ardhi | Uratibu wa Shughuli za Mipango na Utawala | Idara ya Mipango na Rasilimali watu | 3,557,337,588 | 2,375,673,100 | - | - | **5,933,010,688** |
| | | Uratibu wa Shughuli za Kamisheni ya Ardhi Pemba | Afisi ya Kamisheni Pemba | 344,027,175 | 791,729,328 | - | - | **1,135,756,503** |
| | | **Jumla ndogo** | | **3,901,364,763** | **3,167,402,428** | - | - | **7,068,767,191** |
| | | **JUMLA KUU** | | **5,625,100,000** | **3,167,402,428** | | | **8,792,502,428** |